# Nipashe

**Jumatano Juni 3, 2020** • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580248

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710




## Siri mwizi kukutwa amechapa usingizi kwa mwandishi wa ITV

UKURASA 2



Museveni anavyoitumia corona kuahirisha uchaguzi mkuu 2021

siasa

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Bunge linapokoroma mifugo 'kuporwa na kuyeyuka mfugaji akishinda kesi

Mauzauza kuelekea uchaguzi 2020

• Nyerere aliona...

UKURASA 11

# VIGOGO MSD MBARONI



**NI** madai matumizi mabaya madaraka, kuisababishia serikali hasara, CCM nayo yaiita Takukuru...

*Endelea ukurasa 2*

Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbung'o.

## BAA LA CORONA



Kunapoandaliwa tamasha la mkusanyiko wa watu, hakuna haja ya kuchukua kipimo cha corona, isipokuwa mtu yeyote anayejisikia homa au dalili, asiruhusiwe kushiriki. WHO

* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## WAZIRI AMSHTAKI DC KWA JPM MADAI UTORO

UKURASA 7

# ACT yaanika dosari 3 maadili ya uchaguzi

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store



**MICHEZO** MMACHINGA ASHUKIA WAZAWA KASI KAGERE UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Vigogo MSD mbaroni tuhuma za rushwa

**Elizabeth Zaya na Maulid Mmbaga**

ALIYEKUWA Mtendaji Mkuu wa Bohari ya Dawa nchini (MSD), Laurian Bwanakunu, anashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) kwa tuhuma za rushwa.

Pia, Takukuru inamshikilia Kaimu Mkurugenzi wa Lojistiki wa MSD, Byekwaso Tabura.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, jijini Dar es Salaam na Ofisa Uhusiano wa Takukuru, Doreen Kapwani, watuhumiwa hao wanashikiliwa na taasisi hiyo makao makuu.

Alisema watuhumiwa hao wamehifadhiwa mahabusu ya ofisi za Takukuru Upanga, jijini Dar es Salaam kuanzia jana kwa ajili ya kupisha uchunguzi.

"Watuhumiwa hawa wanakabiliwa na tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka pamoja na kuisababishia Serikali hasara kinyume na sheria ya kuzuia na kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007," ilibainisha.

**CCM YALIA RUSHWA**

Wakati huo huo, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimeitaka Takukuru, kuwakamata wote wanaozunguka kuwarubuni wananchi kwa rushwa ili wawapigie kura.

Katibu wa Itikadi na Uenezi, Huphrey Polepole, alisema lengo la kutoa rushwa ni ili wapigie kura.

Aidha, chama hicho kimetaka kukamatwa kwa wanaopita majimboni kuchangisha fedha kwa madai kwamba ni ya kuchukulia fomu ya mgombea urais.

Polepole aliitaka Takukuru kuwakamata wanaopita wakidai wametumwa na chama hicho kwenda kufanya utafiti kwa ajili ya kubaini ukubalifu wa wabunge wa CCM.

"Kuna watu wanaopita mikoani, wilayani na majimboni kwa sasa wakisingizia kwamba wanachangisha fedha kwa ajili ya fomu ya mgombea urais. Sisi tunajua utaratibu wa chama chetu, mgombea wetu mpaka usawa huu anajulikana na ni desturi ya chama chetu, tunaomba sana matapeli na walaghai wanaofanya hivyo wakamatwe," alisema Polepole.

"Utafiti chama hiki kinafanya chenyewe kawa taratibu mahsusi na kina kitendo chake kinachofanya kazi hizo za utafiti kwa weledi, hao wanaojipatia hawana kibali, wapuuzwe na vema Takukuru ikawafuatilia na kuwakamata," aliongeza.




Kamishna wa Idara ya Uhamiaji nchini, Dk. Anna Makakala, akinyanyua ufunguo juu kuonyesha furaha yake, baada ya kukabidhiwa nyumba 103 na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), katika eneo la Iyumbu, jijini Dodoma jana. Wanaoshuhudia ni Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa na (kushoto) ni Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Siri mwizi kukutwa amechapa usingizi kwa mwandishi ITV

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KIJANA anayedaiwa kuwa mwizi aliyetambulika kwa jina la Daudi Suleiman maarufu kama 'Kiboko', amejikuta amelala katika gari la mwandishi wa habari wa ITV Zanzibar, Farouk Karim, ikidaiwa aliingia katika gari hilo kwa lengo la kutaka kuiba.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi ambapo kijana huyo akiwa na vitu mbalimbali alivyoviiba, alinasa katika gari hilo na kulala usingizi usiku kucha bila kujitambua.

Akizungumza na Nipashe, Farouk Karim alisema kuwa kijana huyo aliingia katika nyumba yake kwa kuruka ukuta na kuiba vitu mbalimbali.

Pia alibainisha kwamba mtuhumiwa huyo alivunja gari lake na kutaka kuiba, lakini alinasa akiwa ndani ya gari na kulala humo hadi asubuhi.

Nipashe ilimuuliza Farouk aliweka mtego gani ambao ulimfanya mwizi huyo kunasa, alisema yeye hana mtego wowote aliotumia, isipokua ni kumwamini Mungu.

"Mimi sina dawa yoyote niliyotumia, Mungu tu kataka kumuadhiri kijana huyo ambae ni mwizi maarufu hapa mtaani petu Fuoni," alisema.

Alieleza kuwa kijana huyo kwa sasa anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa hatua zengine za kisheria.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Simon Pasua, alisema kuwa Jeshi la Polisi linamshikilia kijana huyo, na uchunguzi utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

## PM akabidhi nyumba 103 Idara Uhamiaji

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekabidhi nyumba 103 zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 5.6 kwa Idara ya Uhamiaji nchini na kuagiza zitunzwe na mazingira ya eneo hilo.

Pia, amelitaka Shirika la Nyumba nchini (NHC), kuchangamkia soko kwa kujenga nyumba zaidi mkoani Dodoma kutokana na serikali kuhamishia shughuli za serikali jijini hapo.

Nyumba hizo zimejengwa eneo la Iyumbu na kununuliwa na serikali ambayo imezikabidhi idara hiyo.

Akizungumza jana kwenye makabidhiano hayo, Waziri Mkuu aliwataka kuzitunza nyumba hizo pamoja na mazingira yanayolizunguka eneo hilo.

Alisema soko la nyumba bado linahitajika sehemu kubwa Dodoma kutokana na ujio wa serikali na watumishi wengi wamehamia mkoani humo.

Aliwataka NHC kujenga nyumba nyingi zitakazoendana na uhitaji ya sasa kwa kuzingatia hali za Watanzania.

Naye, Mkurugenzi wa NHC, Dk. Maulidi Banyani, alisema makabidhiano hayo ni ya awamu ya pili ambayo ni nyumba 40 na awamu ya kwanza zilikabidhiwa nyumba 63.

Dk. Banyani alisema shirika hilo limejenga nyumba 201 katika eneo hilo na idara hiyo imechukua 103, zilizobaki zimeuzwa kwa idara zingine za serikali.

Hadi kukamilika kwa mradi huo, watakuwa wametumia Sh. bilioni 14.3 kwa kujenga nyumba 300 ndani ya eneo hilo na kuwaomba wanaozihitaji kuwasiliana na shirika haraka.

Alisema eneo hilo lina ukubwa wa hekari 234 na kati ya hilo, idara hiyo wamechukua eneo la ukubwa wa hekari 40.

Kwa upande wake, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, alisema nyumba hizo zitawasaidia idara hiyo kwa sababu zimewaweka askari wao mahali pamoja jambo linalo rahisisha kupatikana kwao wakati wote.

## HABARI KITAIFA

# Mtoto matatani tuhuma za mauaji ya baba yake

Na Christina Haule, MOROGORO

MKAZI wa Wilaya ya Gairo, Yohana Lameck (17), anashikiliwa na polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kumuua baba yake mzazi Issaya Lameck (47) kwa kumpiga ngumi na kumkanyaga sehemu mbalimbali za mwili wake kutokana na ugomvi baina yao.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, mauaji hayo yalitokea Mei 31, majira saa 12 asubuhi, katika kitongoji cha Manyani Kata ya Mkalama.

Kamanda huyo alifafanua kuwa kabla ya mauaji hayo, Mei 30, majira ya saa 12 jioni, baba huyo alirudi nyumbani kwake akiwa amelewa ndipo ukazuka ugomvi na mtoto wake huyo ambaye alimpiga ngumi baba yake sehemu za usoni na kudondoka chini kisha kuendelea kumkanyaga sehemu za tumboni hali iliyosababisha kupata maumivu makali mwilini.

Alisema baada ya tukio hilo ndugu wa marehemu waliamua ugomvi na hawakuweza kumpatia msaada wa kimatibabu kutokana na hali ya ulevi na kwa kuwa mwenyewe kabla hajafa alidai hajaumia, lakini siku iliyofuata Mei 31, alizidiwa na kufariki dunia.

Kamanda Mutafungwa alisema mwili wa marehemu umeshafanyiwa uchunguzi wa kidaktari na kukabidhiwa kwa ndugu wa marehemu kwa mazishi.

Alisema mtuhumiwa huyo anaendelea kushikiliwa na polisi na upelelezi ukikamilika atafikishwa mahakamani kujibu shtaka lake la mauaji.

Wakati huo huo, Nuru Hassan (35), mkulima na mkazi wa Kasiki wilayani Kilosa, mkoani hapa anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kupatikana na nyara za serikali.

Kamanda Mutafungwa alisema, tukio hilo lilitokea Juni Mosi majira ya saa moja asubuhi katika kitongoji cha Kisiki, Tarafa na Wilaya ya Kilosa, askari polisi kwa kushirikiana na askari wanyamapori wa Hifadhi ya Mikumi wakiwa doria na misako walipokea taarifa za kuwapo kwa mtu mwenye nyara za serikali na walipofuatilia walimbaini mwanamke huyo.

Alisema walifika nyumbani kwake na baada ya upekuzi ndani ya nyumba walikuta jino la ndovu lenye uzito wa kilogramu 7.5 lenye thamani ya Sh. 34,635,000, likiwa limehifadhiwa kwenye mfuko wa salpheti na kufichwa katika uvungu wa kitanda chake.

Alisema mtuhumiwa huyo anaendelea kuhojiwa na hatua za kufikishwa mahakamani zitachukuliwa.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala, akizungumza na waandishi wa habari katika Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro, ndege ya kwanza ya abiria ilipotua jana baada ya miezi mitatu ya tishio la Covid 19. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godfrey Mollel. **PICHA: MARC NKWAME**

# ACT yaanika dosari maadili ya uchaguzi

Na Mary Geofrey

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimebainisha upungufu uliomo kwenye Rasimu za Kanuni za Uchaguzi zilizowasilishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa vyama vya siasa.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alibainisha upungufu huo jana katika taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Alitaja upungufu huo ni mawakala kunyimwa hati za viapo kupitia rasimu ya kanuni zote mbili ya uchaguzi wa madiwani na ya uchaguzi wa wabunge na Rais.

"Kanuni zote zimeweka utaratibu wa wasimamizi wa uchaguzi kutuma orodha na utambulisho wa mawakala kwa wasimamizi wa vituo. Kwa uzoefu, utaratibu huu utatumika kuwahujumu mawakala wengi wa vyama vya upinzani. Wasimamizi wa uchaguzi wasio waadilifu watatumika kutowasilisha majina ya mawakala wa vyama vya upinzani," alisema Shaibu.

Kadhalika, alisema pia mawakala hawatapewa nakala za matokeo, na kwamba kupitia rasimu za kanuni hizo zinasema, mawakala wa vyama vya siasa kupewa nakala za matokeo.

Alifananua zaidi kuwa kanuni hizo zinasema nakala za matokeo zitatolewa iwapo kutakuwa na nakala za kutosha kupitia (Kanuni ya 56 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani na kifungu cha 63(2) cha Kanuni za Uchaguzi wa Wabunge na Rais.

"Swali la kujiuliza ni kuwa NEC haikujiandaa kwa uchaguzi? Haina hata fedha za kuzalisha nakala za kutosha na kuepusha mizozo isiyo ya lazima?" alihoji Shaibu.

Alitaja kipendele kingine ni waangalizi wa uchaguzi kuzibwa mdomo, na kwamba kupitia rasimu za kanuni za uchaguzi zinatumia lugha ya hiyari kwa NEC kuwaalika waangalizi wa kimataifa.

Alisema kanuni hizo pia zinakataza waangalizi wa kimataifa na wa ndani kuripoti kwa vyombo vya habari upungufu wa uchaguzi watakaouona wakati uchaguzi ukiendelea kupitia Kifungu cha 20(2)(j) cha Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani na Kanuni za Wabunge na Rais.

Shaibu anasema pia na mfumo mbovu wa kuwajibisha wasimamizi wa uchaguzi katika Rasimu ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani kupitia Kanuni ya 66(1) na kifungu cha 74(1) cha Kanuni za Uchaguzi wa Wabunge na Rais zinatamka kuwa iwapo Msimamizi wa Uchaguzi atakwenda kinyume cha Kanuni za Uchaguzi, Mkurugenzi wa Uchaguzi atamtaka Waziri mwenye dhamana kuchukua hatua za kinidhamu.

"Suala la kuwawajibisha wasimamizi wa uchaguzi linapaswa kuachwa mikononi mwa NEC pekee. Waziri ambaye ni kada wa CCM hawezi kuchukua hatua stahiki dhidi ya wasimamizi wa uchaguzi," alisistiza Shaibu.

Kupitia upungufu huo, ACT- Wazalendo imeitaka NEC ishirikishe wadau vya kutosha kabla ya kufanya marekebisho ya Kanuni za Uchaguzi, na ni muhimu kwa NEC kufanya kikao cha wadau na kujadiliana juu ya mabadiliko ya Kanuni kabla ya kufanya mabadiliko hayo.

Shaibu aliitaka NEC pia iepushe nchi na machafuko yasiyo ya lazima kwa kuhakikisha inaondosha vifungu ambavyo vitahatarisha amani ya nchi.

Hivi karibuni, malalamiko kama hayo, yalitolewa na Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema ), John Mnyika , ambaye hata hivyo alikiri kusaini maadili hayo kwa maelezo kuwa wataendelea kuzipinga ili kuepuka kukosa kushiriki uchaguzi iwapo chama cha siasa hakitasaini kanuni hizo kama iliyoelezwa katika rasimu ya kanuni hizo .


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AccessBank Tanzania Limited** imetoa idhini kwa **DESTENI COMPANY LIMITED** wake kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara, Magari, Nyumba na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kua utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) kwa dhamana ya nyumba au kiwanja. Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada kwa siku husika iliyopangwa. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | LUMUMBA | DESTINI COMPANY LTD | MMASSY/B,FRANK | MMASSY/B,FRANK | HOUSE | MICHUNGWANI | 20/6/2020 |

**MASHARTI YA MNADA**

Dhamana zitauzwa mahali zilipo. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer), na salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada. Malipo yote yanayohusu nyumba ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

MAWASILIANO: ACCESSBANK TANZANIA – 0677 860 000

215759902

# Makonda aagiza daladala kusimamisha wanafunzi

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameagiza daladala za mkoa huo, ziruhusu wanafunzi wanne kusimama ili kuondoa changamoto ya usafiri.

Makonda alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akipokea vifaa tiba na vifaa vya ujenzi na kueleza kuwa, agizo hilo la kubeba wanafunzi lianze mara moja.

"Sitaki kusikia mwanafunzi anaachwa eti konda na dereva wanasema wanabeba abiria kulingana na viti, wabebwe ili waende kwenye masomo," alisema.

Alisema daladala litakalokuwa limebeba wanafunzi wasiozidi wanne, trafiki haruhusiwi kulikamata, lakini kama amesimamisha abiria wachukue hatua.

Pia, alisema alitoa maelekezo ya bodaboda na bajaji kuingia katikati ya jiji kubeba abiria, lakini kuna mtu mmoja ameanza kuwakamata na kumweleza kuwa hakuna Mkuu wa Mkoa mwingine.

"Hakuna Mkuu wa Mkoa mwingine, nipo na bado nipo, bodaboda, bajaji mnaendelea kuingia katikati ya mji kuendelea na shughuli zenu za kiuchumi kama nilivyoelekeza kauli hii sijaitengua na hakuna mwingine wa kuitengua katika mkoa huu labda mamlaka nyingine kutoka juu yangu," alisema.

Makonda aliwaeleza hao wanaendesha ukamataji huo wakiendelea atawakamata na kuwatia ndani.

Alisema kuna mabati 1,000 ambayo watapewa wajane waliobomokewa nyumba zao kipindi cha mvua kujenga upya nyumba hizo, lakini zisiwe bondeni.

"Wenyeviti wa mitaa taarifa zao mzikamilishe mzikabidhi kwa Mkuu wa Wilaya ili haya mabati yaliyopo yaweze kukabidhiwa kwenu," alisema.

Alilishukuru Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa kuendelea kuitunza michango wanayoipata.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Ilala, Zuberi Chembera, akimkabidhi Koplo Brown Twaibu cheti cha pongezi kwa kazi njema aliyoifanya ya kuelimisha jamii juu ya uvaaji wa barakoa kwa dhumuni la wananchi kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona, katika hafla iliyoandaliwa na benki ya NBC, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtoto auawa kwa kushambuliwa na fisi

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MTOTO mwenye umri wa miaka miwili, Charles Makilika, ameuawa baada ya kushambuliwa na fisi usoni katika kitongoji cha Mwagala, Ugweto Manispaa ya Shinyanga.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema tukio hilo limetokea Juni mosi, majira ya saa moja jioni, wakati mtoto huyo akicheza na wenzake.

Alisema wakati akiendelea kucheza, ghafla fisi alitokea na kumshambulia usoni kwa kumng'ata na kumburuza umbali wa mita 50 na kumsababishia majeraha makubwa yaliyosababisha kuvuja damu nyingi na kupoteza uhai.

"Fisi huyo alimburuza umbali wa mita 50, alimwachia baada ya kusikia kelele za watu waliokuwa wakimfukuza," alisema Magiligimba.

"Mtoto huyu alifariki dunia njiani wakati akikimbizwa katika Hospitali ya Rufani Bugando, jijini Mwanza," alisema.

Kamanda alitoa wito kwa wananchi mkoani humo, kuchukua tahadhari kwa watoto wao kuhakikisha wanacheza katika maeneo salama, hasa katika kipindi hiki ambacho fisi wamezagaa katika maeneo mbalimbali.

Mkoa wa Shinyanga, yameshatokea matukio sita ya wananchi kujeruhiwa na wanyama aina ya fisi, huku watoto watatu wakipoteza maisha.

# Asilimia 90 wanafunzi kidato cha 6 waripoti

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Gerald Mweri, amesema kuwa zaidi ya asilimi 90 ya wanafunzi wa kidato cha sita wameripoti katika shule zao hadi kufikia jana asubuhi na kuanza masomo.

Amesema katika shule za serikali wanafunzi hao watakuwa na mitihani ya kuwapima kabla ya kuingia kwenye mtihani wa taifa Juni 29, mwaka huu.

Mweri, alisema mtihani huo utawasaidia walimu, kubaini upungufu wa wanafunzi katika mada mbalimbali na kufanyia kazi.

Alisema baada ya mitihani hiyo, walimu watafanya tathimini katika maeneo ambayo wanafunzi wana upungufu ili kuwasaidia kujiweka sawa kabla ya kuingia katika mtihani wa mwisho.

"Kesho (leo) katika shule zetu nyingi za serikali watakuwa na mitihani mkoa kama Lindi na Mtwara, wanafunzi wa kidato cha sita watakuwa na mitihani ya kuwapima ili kubaini maeneo yenye upungufu na kwa muda wa wiki mbili baada ya mitihani walimu watakuwa na kazi ya kufanyia kazi upungufu huo," alisema Mweri.

Pia, alisema kabla ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kutangaza shule pamoja na vyuo kufungwa Machi 17, wanafunzi wa kitado cha sita walikuwa tayari wamesha maliza mada zao zote.

"Watu wanafikiri kuwa watoto hawa, walikuwa bado hawajamaliza topic zao, lakini ukweli ni kuwa tayari walisha maliza na hivi sasa kitakacho fanyika ni kuwapatia mitihani hii na walimu kuendelea kusimamia na kuwasaidia kubaini upungufu kwa siku hizi 28 zilizobaki kuingia katika mtihani," alisema Mweri.

Vile vile, alisema mpaka sasa hakuna mwanafunzi aliyeripotiwa kukutwa na maambukizo ya virusi vya corona, hivyo wazazi wawe watulivu na kuondoa wasiwasi.

Aliwaagiza maofisa elimu wote wa wilaya pamoja na mikoa, kuwachukulia hatua kali, wamiliki wa shule ambao wataoneka kwenda kinyume na muongozo uliotolewa na serikali.

"Kuna shule nilisikia kuwa walikuwa wana 'spray' (kupulizia dawa) wanafunzi, nimeagiza waende kulishughilikia jambo hili, kwani ni lazima wafuate muongozo kama unavyosema, tumeusambaza katika maeneo mengi wanaweza kuendelea kuusoma," alisema.

"Spirit ni marufuku, kwanza hii ni kilevi, lakini pia inaweza kusabaisha milipuko ya moto katika mabweni ya shule zetu hivyo ni marufuku, wanafunzi wanawe mikono kwa maji na sabani na kuacha kutumia vitakasa mikono vya kienyeji ambavyo havikidhi viwango vya kitaalamu," alisema.

Aliagiza shule zote kuendelea kuzingatia tahadhari zote, kama ilivyo shauriwa na Wizara ya Afya, kwa kuweka maji ya kunawa na sabuni, uvaaji wa barakoa pamoja na kukaa kwa umbali unaoshauriwa.

# TANGAZO

## DEPOSIT INSURANCE BOARD

## TANGAZO KWA UMMA

**KATIKA SHAURI LA MBINGA COMMUNITY BANK PLC, COVENANT BANK FOR WOMEN (T) LTD, EFATHA BANK LTD, KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LIMITED, MERU COMMUNITY BANK NA NJOMBE COMMUNITY BANK LIMITED (ZILIZO CHINI YA UFILISI)**

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa zilizokuwa;

1. **Mbinga Community Bank Plc,**
2. **Covenant Bank for Women (T) Ltd,**
3. **Efatha Bank Ltd,**
4. **Kagera Farmers Cooperative Bank Limited,**
5. **Meru Community Bank Limited na**
6. **Njombe Community Bank Limited, kwamba;**

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia matawi yote ya benki ya TPB Bank Plc yaliyopo nchini.

2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 37.91% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.

3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia zao kufika kwenye tawi lolote la benki ya TPB Bank Plc ili kulipwa fidia zao.

**UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 28 MEI 2020**

**MKURUGENZI**
**DEPOSIT INSURANCE BOARD**
**JENGO LA MAKAO MAKUU YA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**
**2 MTAA WA MIRAMBO**
**GHOROFA YA 11,**
**MNARA WA KASKAZINI**
**11884 DAR ES SALAAM**

**BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ**
**SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390**
**Fax: +255 22 223 4200**

## DEPOSIT INSURANCE BOARD

## TANGAZO KWA UMMA

**KATIKA SHAURI LA FBME BANK LIMITED (ILIYO CHINI YA UFILISI)**

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa iliyokuwa FBME BANK LIMITED kwamba;

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam.

2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 51.77% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.

3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia ya bima ya amana, kufika kwenye yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam ili kulipwa fidia zao.

**UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 28 MEI 2020**

**MKURUGENZI**
**DEPOSIT INSURANCE BOARD**
**JENGO LA MAKAO MAKUU YA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**
**2 MTAA WA MIRAMBO**
**GHOROFA YA 11,**
**MNARA WA KASKAZINI**
**11884 DAR ES SALAAM**

**BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ**
**SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390**
**Fax: +255 22 223 4200**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kama hatuzibi ufa corona tunaelekea kujenga ukuta

TUTAFAKARINI corona na kujiepusha na utani, ndiyo ushauri ambao tunaoutoa kutokana na kurudi nyuma jitihada za kujihadhari na Covid -19.

Tunayasema haya kwa sababu watu wengi hawajali hasa jijini Dar es Salaam eneo lililokuwa kitovu cha corona.

Inasikitisha kuona kuwa wengi wanapuuza kuvaa barakoa, kusongamana na pia hata kampeni za kunawa zimepungua.

Tunayasema haya baada ya kufanya uchunguzi kwenye daladala na kubaini kuwa umma umeacha matumizi ya barakoa.

Si hivyo tu, hata kwenye minada na masoko iwe barabarani au kwenye vituo vya basi hali ni hiyo hiyo, uvaaji barakoa umeachwa na mazoea ya kujikusanya na kukaribiana yanarudi kwa kasi.

Aidha, tunaona kuwa katika sehemu mbalimbali kampeni za kunawa na kuweka ndoo za maji na kusisitiza watu kusafisha mikono kabla ya kuhudumiwa au kusikilizwa zinaanza kudorora.

Wengi wanajibu kwa kujiamini kuwa 'corona imekwisha', imeondoka na kwamba hakuna watu wanaoumwa au pia sijafiwa au kuona mtaani kwangu misiba ya corona'.

Kupuuza maradhi haya kumekithiri vijiweni hasa kwenye mikusanyiko ya waendesha pikipiki, bajaji na vituo vikuu vya mabasi kuanzia Ubungo, Mbezi, Makumbusho na Kariakoo.

Ulevi kwenye sehemu za buruduni unaanza kukolea. Watu wanakunywa pombe kwa kujisahau, wahudumu nao hawana tahadhari. Hubeba chupa kwa kushika mdomoni ambako mteja amemaliza kunywa na bila kujali wanachukua chupa nyingine na kufungua hata kabla ya kunawa wala kutumia vitakasa mikono.

Hiyo ni hatari nyingine inayoweza kutokea wakati huu ambao watu wanaamini kuwa corona imekwisha. Hakuna sababu ya kujidanganya ugonjwa upo na kama wananchi wanadai kuwa hawajaona waliopoteza maisha ni vizuri viongozi wa mikoa na wilaya wakaanza kampeni upya kuwahamasisha kubadilika.

Ni wazi kuwa huenda kinachotokea Dar es Salaam ndicho kinachoonekana Tanzania nzima. Kupuuza corona. Kujiamini kupindukia na kujipa ushindi wa vita usiokuwa na ukweli .

Tunaona kuwa si jambo la kupuuza tena. Kuna haja ya kuwahamasisha watu kuacha kubweteka na kujiachia kwa kuwa kasi ya kuambukiza corona ni ya ajabu na ya kutisha.

Virusi vinaathiri watu wengi kwa muda mfupi na kusambaa kwa kasi ya ajabu na kusababisha maafa makubwa kuliko ambavyo watu wanadhani.

Tunawashauri viongozi kufuatilia na kuweka kanuni za kubadili tabia ikiwamo kuwapo na usimamizi wa kuvaa barakoa kwenye magari ya daladala, mwendokasi na bodaboda pamoja na bajaji.

Aidha, kupunguza misongamano na kuweka umbali wa zaidi ya mita mbili kati ya mtu na mtu ni jambo la kuhimizwa na hata kupunguza misongamano masokoni kwa kuwatafutia wajasiriamali maeneo mengi zaidi ya kuuza bidhaa zao.

Ni vyema pia kuhimiza uvaaji wa barakoa kanisani na kuweka umbali wa mita mbili kati ya waumini na kudhibiti msongamano wakati wa utoaji wa sadaka au kushiriki chakula cha Bwana kwenye makanisa.


Ni vyema pia kuwahimiza wanaotumia usafiri wa umma kubadili nguo wanazovaa kwenye mabasi mara moja wanaporudi nyumbani, badala ya kuingia nazo ndani na kukaa kwenye viti sabuleni au vitani kwani pia hiyo inaweza kuwa njia ya kusambaza virusi nyumbani.

Nguo hizo zihifadhiwe sehemu na kufuliwa haraka iwezekanavyo kwani tahadhari ni muhimu kuliko kuendelea kupuuza.

Kuhimiza usafi na kunawa mikono kwenye sehemu za sokoni, vituo vya mabasi, nyumba za ibada na kuhakikisha kuwa maji na sabuni vinakuwapo kwani kama si kuziba ufa Watanzania watalazimika kujenga nyumba kwa gharama kubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Makada wa mtindo huu wamekalia kuti kavu



Na Sabato Kasika

WAKATI huu ambao nchi inaelekea katika uchaguzi mkuu, viongozi waandamizi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamekuwa wakitoa tahadhari kwa makada wake, ili kuepuka kutumia njia ya mkato kupata uongozi.

Viongozi wa chama hicho wanasema, wako macho dhidi ya wanachama wao, ambao wanavuruga kabla ya uchaguzi huo kwa lengo la kupata viongozi wanaofaa kukiwakilisha.

Kwamba, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, CCM ilichelewa kuwaengua baadhi ya wanachama waliovuruga na kuigawa kwa maslahi binafsi, lakini uchaguzi wa mwaka huu itawaengua mapema.

Hii ni kwa mujibu wa Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, akisema kwamba CCM ilichelewa kuwaondoa wasiofuata taratibu za chama, na kusababisha wakigawe chama, lakini sasa wamewadhibiti.

Anasema, hawawezi kujitokeza tena katika uchaguzi ujao na kwamba walioanza kujipitisha kwenye majimbo na kukusanya watu kufanya vikao au kutoa rushwa, hao tayari 'vichwa vyao vimeliwa'.

Katika kuhakikisha chama kinapata wawakilishi halali, Polepole anasema, mwaka huu kuna mfumo madhubuti wa kupokea taarifa kwa walioanza kampeni mapema kinyume na utaratibu.

Anasema watakaobainika hawatapitishwa na chama hicho kwenye kura za maoni, hivyo ni wazi kwamba 'wamekalia kuti kavu'.

Siyo mara ya kwanza chama kutoa kauli kama hiyo, alianza Makamu wa Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Philip Mangula, Katibu Mkuu Dk. Bashiru Alli, akasisitiza.

Hivyo ni wakati wa makada wa CCM kusoma ishara za nyakati na kutambua kuwa chama chao hakitaki makandokando bali taratibu zifuatwe ili kupata wagombea waliopitishwa kihalali katika kura za maoni.

Utafutaji wa dhamana ya chama kihalali unamjengea mtu heshima, hivyo ni muhimu wahusika wakazingatia hilo kama wana nia ya kweli ya kuwatumikia wananchi kwenye nafasi mbalimbali za uongozi.

Kada wa CCM anaweza kupenya kwa kutumia njia ya mkato bila mifumo ya chama kumbaini, lakini mwishowe ataongoza kiujanjaunja na kushindwa kuleta maendeleo, kwa vile nafasi ameipata kupitia njia hiyo.

Ninaamini kwamba kutafuta uongozi kwa kufuata taratibu zilizowekwa kunaweza pia kuepusha makada kukumbana na changamoto mbalimbali zikiwamo za kunaswa katika mitego iliyowekwa na chama.

Vinginevyo wanaong'ang'ania njia za mkato watajikuta wamekalia kuti kavu na hatimaye kukosa uongozi, kutokana na ukweli kwamba hata Katibu Mkuu alishasema chama kinatafuta viongozi siyo warembo.

Kwa maana hiyo wale ambao wameanza kujipitisha kwa wanachama ni sawa na mrembo kujipitisha mbele ya watu ili wamuone, lakini kwenye suala la kutafuta uongozi ni kufuata utaratibu.

CCM inaamini kwamba hadhi yake kwa wananchi, imesharejea, hivyo haitaki makada wa kukiharibia na kuirudisha nyuma, badala yake wafuate taratibu wanaposaka kuongoza.

Ni wazi kada mwenye uwezo wa kuongoza atachaguliwa bila kutumia mbinu, ambazo zinakwenda kinyume na taratibu na kalenda ya chama hicho tawala.

Hivyo kila mwanachama anayetaka nafasi katika uchaguzi mkuu, apitie katika mchakato halali wa kura za maoni ndani ya chama chake, hatimaye apewe nafasi ya kukiwakilisha chama dhidi ya wagombea wa vyama vingine.

CCM ni miongoni mwa vyama vikongwe barani Afrika na hilo halina ubishi, lakini wanapojitokeza makada wanaotumia mbinu zisizofaa kwa lengo la kupata uongozi, wanakiharibia mbele ya umma.

Mkazo unaowekwa na viongozi wa CCM ni kuwataka wanachama kufuata, ni wazi wamedhamiria kuhakikisha chama kinapata wawakilishi wanaokubalika na wenye uwezo wa kuwatumikia Watanzania.

Kuna msemo wa Kiswahili kwamba; 'kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza', hivyo watu wenye nia ya kuwatumikia wananchi hawezi kuanza kuzunguka katika kata na majimbo kufanya kampeni kabla ya muda.

Badala yake watasubiri kalenda ya chama, ambayo ina taratibu zote zinazotakiwa kuzingatiwa, ili hatimaye wapate wawakilishi wanaokubalika na wote.

# Takukuru yakamata makada 18 CCM tuhuma za rushwa

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Mtwara, imewakamata watu 18 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), akiwamo mtia nia Jimbo la Masasi kwa tuhuma za rushwa kuelekea uchaguzi.

Mtia nia huyo ni Ofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Dar es Salaam, Muhaji Mrope (CCM) na wenzake pia wanatuhumiwa kuitisha vikao kinyume na taratibu.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Mtwara, Enock Ngailo, juzi ofisi yake ilipokea taarifa kutoka kwa msiri wao ikielezea kuwa siku hiyo (Juni mosi) kutafanyika vikao viwili.

"Kikao cha kwanza kimefanyika nyumbani kwa Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kata ya Mlingula muda wa saa 3:00 asubuhi na kingine kinafanyika nyumbani kwa Mwenyekiti wa CCM, tawi la Mlingula saa 5:00 asubuhi," alisema.

Alisema taarifa hiyo ilieleza kuwa vikao vyote hivyo vimefanyika kwa lengo la kuwashawishi wajumbe watakaopiga kura za maoni kuwachagua wagombea ubunge Jimbo la Ndanda, Wilaya ya Masasi.

Pia alisema taarifa hiyo ilieleza kuwa viongozi hao kwa maana ya Katibu Mwenezi CCM, kata ya Mlingula, Martine Chinemba na Mwenyekiti wa CCM, tawi la Mlingula, Hussein Bwanali ni mawakala ambao wanatumiwa na Mrope aliyeonyesha nia ya kugombea ubunge Jimbo la Ndanda, uchaguzi ujao.

Ngailo alisema baada ya ofisi yake kupokea taarifa hiyo, maofisa wa Takukuru Wilaya ya Masasi walifika eneo la tukio ni nyumbani kwa Bwanali, maarufu kama 'DJ' mtaa wa Tandika, kata ya Mlingula.

Alisema walipofika walikuta mtia nia huyo, mawakala wake pamoja na wajumbe wakiwa katika kikao hicho na kuwaweka chini ya ulinzi watu wote 18 na kuwafikisha katika ofisi za Takukuru, Wilaya ya Masasi kwa mahojiano. "Baada ya mahojiano watuhumiwa 16 ambao walikuwa ni wanachama, wajumbe na baadhi ya viongozi waliachiwa kwa dhamana jana (juzi).

"Watuhumiwa wengine ambao ni mtia nia Mrope na Katibu Mwenezi CCM, kata ya Mlingula Chinemba, waliwekwa mahabusi Kituo cha Polisi, Wilaya ya Masasi wakati uchunguzi ukiendelea na wameachiwa kwa dhamana leo (jana)."

# Jafo kumshtaki DC kwa Rais Magufuli

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**



WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (pichani), amemshukia Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Dk. Halfan Haule, baada ya kuzidisha siku za likizo.

Inadaiwa kuwa Dk. Haule aliomba likizo ya siku 14, lakini akaamua kukaa zaidi ya mwezi mmoja bila ya kutoa taarifa.

Akizungumza jana katika kikao kilichofanyika katika ukumbi wa Manispaa ya Sumbawanga, Jafo alisema kitendo alichokifanya mkuu huyo wa wilaya kinaonyesha utovu wa nidhamu kwa watumishi katika wilaya yake.

Alisema kuwa pamoja na kitendo hicho, Ofisi ya Tamisemi ilimwandikia barua ili kumpa nafasi ajieleze kwa nini alifanya hivyo, lakini bado amekaa kimya kana kwamba hakufanya kosa lolote.

"Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga aliomba likizo ya siku 14, lakini akakaa zaidi ya mwezi mmoja bila kutoa taarifa, na hata ofisi ya Tamisemi ilipo mwandikia barua hajajibu mpaka leo, na bado katika wilaya yake ndiko kuna matumizi mabaya ya fedha za serikali na hakuna hatua zilizochukuliwa," alisema Jafo na kuongeza;

"Nitakwenda kumwambia Rais Magufuli maana yeye ndiye mwenye mamlaka ya uteuzi achukue hatua katika hili, hatuwezi kuendelea kuwafumbia macho viongozi wa namna hii, tunataka maendeleo kwa kasi kubwa, na viongozi ndiyo wanapaswa kuwa mfano," alisema Jafo.

Aidha, Jafo amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, kusimamia nidhamu kwa baadhi ya viongozi wa mkoa huo, licha ya kuwa yeye kufanya vizuri, lakini anakwamishwa na viongozi hao wenye kiburi na watovu wa nidhamu.

Akiwa mkoani Rukwa katika Manispaa ya Sumbawanga, Jafo alikagua maendeleo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni stendi kuu ya mabasi ya Sumbawanga Mjini, pamoja na kuweka jiwe la msingi, stendi ya malori ya mizigo iliyopo eneo la Utengule - Manispaa ya Sumbawanga.

Pia alizindua barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 10.55.


NDC

**NATIONAL DEVELOPMENT CORPORATION**

**TENDER No. PA/068/NDC/2019/2020/INV/01**

**PRE-QUALIFICATION FOR DEVELOPMENT AND IMPLEMENTATION OF THE MAGANGA MATITU IRON ORE PROJECT**

**RE-ADVERTISEMENT**

**1. INTRODUCTION**

The National Development Corporation (NDC) was established as a statutory body by an Act of Parliament in 1962, wholly owned by the Government of the United Republic of Tanzania, charged with responsibility of promoting economic development in Tanzania in partnership with the private sector.

The NDC is mandated by the Government of Tanzania to develop projects in the Mtwara Development Corridor. Liganga Iron Ore (Liganga Concession) project, located in Ludewa District in Njombe Region is among anchor projects in the Mtwara Development Corridor. Maganga Matitu is one of the five hills of the Liganga Iron Ore Project set aside by the Government for Local Program to produce sponge iron as raw material to steel industries. The Maganga Matitu iron ore project has an area of 19.63 sq.km for development and implementation of iron ore mine while beneficiation plant and the associated infrastructure might be located in the same area or nearby depending on the outcome of the study. Further, the Government directed NDC to procure an investor who will partner with the Corporation for development and implementation of the Maganga Matitu Iron Ore Project.

**2. OBJECTIVE**

The main objective is to secure experienced and competent investor who will partner with NDC in the development and implementation of the Maganga Matitu Iron Ore Project. The investor or firm is free to form joint ventures/consortia to express the interest.

**3. PROPOSED PROJECT**

The NDC intends to pre-qualify experienced and competent investors and/or firms to act as co-sponsors and shareholders alongside the NDC in promoting a joint venture company which will have the right to develop and implement the Project. This will likely involve:

- exploration and identification of the quantity and quality of the iron ore deposit at Maganga Matitu, including evaluation of the mineralogy and metallurgical response to any separation techniques to be employed, with a view to the subsequent commercial development of an iron ore mine and beneficiation plant; and
- the development of an efficient method for exploiting the deposits having in mind the infrastructural needs of the region including the Mtwara Development Corridor, and the aim of providing through any processing or industry, the maximum amount of "value added" within Tanzania.

**4. INTERESTED INVESTORS**

The NDC now seeks eligible investors to submit their application for pre-qualification for the above-mentioned Project. The interested developers, mining companies, beneficiation companies and/or firms must provide information indicating that they are qualified to be strategic partner by submitting profile of company/consortium, technical and financial capability (including audited Financial Statement for the past 3 years), as well as the experience and past performance of similar business (include CVs of key personnel), of the prospective investors/firms. The evaluation criteria will take into consideration on the above-mentioned items.

**5. PRE-QUALIFICATION DOCUMENT**

Pre-qualification must be made by way of submission of a completed set of pre-qualification documents in English. Completed applications for pre-qualification must be submitted in five (5) hard copies (one original plus four (4) copies including electronic copy on CD) in sealed envelopes, and delivered to the address below.

**6. SUBMISSION DEADLINE**

Pre-qualification must be submitted/delivered to the address below at or before **23rd June 2020, at 14:00hrs,** 6th Floor, Room No. 605, clearly marked **"Tender No.PA/068/NDC/2019/2020/INV/01, pre-qualification for Development and Implementation of Maganga Matitu Iron Ore Project"**

7. Late submission of pre-qualification shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

8. The Corporation reserves the right to continue or reject the tendering process without giving reason(s) thereof and shall incur no any liability.

**Managing Director**
**National Development Corporation,**
**Development House,**
**Kivukoni Front/Ohio Street,**
**P. O. Box 2669**
**Dar es Salaam**

215759702



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo (wa tatu kulia), baada ya kuwasili katika Kijiji cha Kyaka, kwenye eneo litakalojengwa chanzo cha maji cha Mradi wa Kyaka Bunazi, wakati wa hafla ya uzinduzi wa ujenzi wa mradi huo, wilayani Missenyi, mkoani Kagera juzi. **PICHA: MOHAMED SAIF**

# Wajumbe CCM kutumia kadi za kielektroniki vikao vya uteuzi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema katika vikao vya mchakato wa uteuzi wa wagombea mwaka huu, zitatumika kadi za kielektroniki kwa wajumbe.

Aidha, kimesema kitatangaza mchakato wa uchaguzi ndani ya chama hicho baada ya kuvunjwa kwa bunge na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutangaza ratiba yake ya uchaguzi.

Aidha, kimepiga marufuku wagombea hususani wa nafasi ya ubunge kutokwenda na maandamano na matalumbeta katika ofisi za chama hicho wakati utakapofika wa kuchukua fomu ya kuomba ridhaa ya kugombea nafasi hiyo.

Kimesema shangwe hizo zitafanywa na mgombea mmoja pekee atakayekuwa amepitishwa kugombea katika eneo husika.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu wa Itikadi na Uenezi, Huphrey Polepole, alisema utaratibu wa uchaguzi wa chama hicho mwaka huu umebadilika tofauti na ilivyokuwa mwaka 2015.

"Uchaguzi wa mwaka huu ni tofauti, mwaka 2015, mgombea alitakiwa kupita kwenye mitaa na kata katika jimbo husika kutangaza kwamba yeye anatakiwa kugombea, lakini mwaka huu tumebadilisha, mgombea atakwenda kwa unyenyekevu siyo kwa mbwembwe," alisema.

Alisema baada ya mchakato wa kuchukua na kurejesha fomu kumalizika, vitaanza kuketi vikao vya kujadili majina na kutoa mapendekezo.

Polepole alisema wagombea watajadiliwa kwa hatua mbili kwa kupita katika mikono ya Kamati ya Siasa ya Jimbo Zanzibar na Kamati ya Siasa ya Wilaya kwa maana ya wabunge, Kamati ya Siasa ya Mkoa, Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa na kisha Halmashauri Kuu ya Taifa, ambayo itafanya uteuzi wa jina moja.

"Majina hayo yatakuwa ni siri kubwa na yatawekwa na mhuri wa moto na kuyarejesha kwenye mkutano wa jimbo ambako ndiko yatapigiwa kura na wajumbe 1,000 na mchakato wote utatengenezewa muhtasari na kurudishwa makao makuu wa CCM kwa ajili ya mchakato wa kuwajadili kwa mara ya pili watu watatu na hata kufikia kupata jina moja," alisema Polepole.

Polepole alisema katika mkutano mkuu mwaka huu, wamejipanga kutumia kadi za kielektroniki ili kudhibiti mamluki kuingia katika mkutano huo.

"Ule mchakato wa mwanzo tulikuwa tunatumia kadi za kitabu ambazo kulikuwa na watu wabaya walizichapa, kwa hiyo kipindi hiki tumeweka utaratibu wa kielektroniki, tutatumia smart kadi au vitambulisho janja, mjumbe atakayeingia kwenye mkutano ni lazima atapitisha kadi yake kuiswap na akidhibitishwa ndipo ataruhusiwa kuingia ndani. Mamluki wasije kwa kuwa wataumbuka," alisema Polepole.

Alisema utaratibu huo utafanyika katika vikao vyao vyote kuanzia kwenye jimbo, wilaya na na mkutano huo mkuu.

Polepole alisema chama hicho hakitaruhusu wagombea ambao ni majangili na wapenda rushwa na kwamba kimejipanga kuwatafuta popote pale wagombea ambao wamejipanga kutafuta uongozi kwa kutumia rushwa.

# Mch. kortini tuhuma kubaka mwanafunzi

**Mwandishi Wetu**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Mlango wa Ukombozi Gairo, mkoani Morogoro, Joseph Gervas (28), amepandishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kilosa, kwa tuhuma za kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi wa kidato cha tatu mwenye miaka 17 (jina limehifadhiwa).

Mtuhumiwa huyo, alifikishwa katika mahakama hiyo jana mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya, Rehema Mayagilo.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka iliyowasomwa mahakamani, mtuhumiwa huyo anakabiliwa na kesi namba cc.117/2020 ya kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi itakaposomwa tena Juni 16, mwaka huu.

Dhamana ya mtuhumiwa huyo ipo wazi na masharti ni mdhamini kuwa na fedha taslimu Sh. milioni moja, hata hivyo, mtuhumiwa alishindwa kutimiza masharti hayo.

# Mawaziri EAC kufanya kikao mtandaoni

**Na Maulid Mmbaga**

MKUTANO wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki, unatarajia kufanyika kesho na keshokutwa, kwa njia ya video.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Kaimu Mkurugenzi wa kitengo cha mawasiliano ya serikali, Sheiba Bulu, mkutano huo utafanyika Dodoma.

Alisema utaanza kesho kwa ngazi ya wataalamu ukifuatiwa na ngazi ya makatibu wakuu keshokutwa na kutafuatiwa na wa baraza la mawaziri siku hiyo hiyo.

"Mkutano utaanza kufanyika saa 9:00 alasiri hadi saa 11:00 jioni, pia pamoja na mambo mengine tutajadili masuala ya fedha ya Jumuiya," alisema.

# Bei ya mafuta yashuka zaidi

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetangaza bei kikomo za mafuta ya petroli na dizeli ambazo zimeendelea kushuka zaidi.

Kwa mujibu wa tangazo la Ewura lililotolewa jana jijini Dar es Salaam, limeelekeza bei hizo mpya kuanza leo na kumetaja kwa sasa mafuta ya petroli kwa bei ya rejareja mkoa wa Dar es Salaam ni Sh. 1,520 na dizeli ni Sh. 1,546 huku mafuta ya taa yakiuzwa Sh. 1,568.

Katika mkoa wa Arusha bei ya rejareja ya petroli ni Sh. 1,711, dizeli Sh. 1,750 na mafuta ya taa ni Sh. 2,044, Dodoma petroli ni Sh. 1,579, dizeli 1,605 na mafuta ya taa ni Sh. 1,627.

"Kilimanjaro mafuta petroli ni Sh. 1,700, dizeli Sh. 1,739 na mafuta ya taa ni Sh. 2,033, Mbeya mafuta petroli ni Sh. 1,627, dizeli Sh. 1,653 na mafuta ya taa ni Sh. 1,675 na Geita mafuta ya petroli ni Sh. 1,685, dizeli Sh. 1,712 na mafuta ya taa Sh. 1,733," lilieleza.

**Katika mkoa wa Arusha bei ya rejareja ya petroli ni Sh. 1,711, dizeli Sh. 1,750 na mafuta ya taa ni Sh. 2,044, Dodoma petroli ni Sh. 1,579, dizeli 1,605 na mafuta ya taa ni Sh. 1,627.**

HABARI KITAIFA

KWA UFUPI

## Igunga yaagizwa makusanyo mil. 365/-

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, ameigiza Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kuhakikisha inakusanya kiasi cha Sh. milioni 365.2, ambazo inadai wadau mbalimbali katika vipindi tofauti.

Fedha hizo zinatokana na mikopo ya asilimia 10 ya vikundi na ule iliotoa kwa Vijana Saccos ambayo haijarejeshwa na fedha nyingine ambazo zilikusanywa na wakala wa kukusanya mapato ya ndani ambayo hayakuwasilishwa katika halmashauri, na kusababisha hoja za kiukaguzi.

Mwanri alitoa agizo hilo wakati wa kikao maalumu cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Igunga la kupitia hoja ya mbalimbali zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2018/19.

Alisema kati ya hizo, Sh. milioni 174.9 ni mikopo ya vikundi vya wanawake, walemavu na vijana ambayo walikopeshwa lakini hadi bado wanadaiwa.

Alisema fedha nyingine ni milioni 95, ambazo zilitolewa kwa Vijana Saccos katika mwaka wa fedha wa 2014/15, ambapo kati ya hizo aliyekuwa Mkuu wa Wilaya wakati huo alitajwa kukopa shilingi milioni 24 na zote hazijarejeshwa.

## Walia kasi watoto kupewa ujauzito

**Na Welingtone Masele, KALIUA**

BAADHI ya wazazi na walezi wilayani Kaliua mkoani Tabora, wameiomba serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria wanaokwamisha kwa makusudi au kumaliza kinyemela kesi za watu wanaotuhumiwa kuwapa mimba watoto wa shule.

Watu hao wamekuwa wakiwasababishia matatizo wakati wa kujifungua pamoja na kuendelea kuwapo kwa mimba za utotoni.

Wakizungumza wakati wa kukabidhiwa mifuko 100 ya saruji na mabati 40 vilivyotolewa na Shirika la Reli nchini (TRC) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Ukumbi-Kakoko iliyopo jirani na eneo jipya la uchimbaji wa kokoto inayowekwa kwenye reli, wananchi hao walisema watoto wengi wilayani Kaliua wanakatishwa masomo kwa kupewa mimba au kuozeshwa, jambo linalokatisha tamaa jamii.

Aidha, walisema baadhi ya wahusika wakikamatwa na kupelekwa katika vyombo vya sheria, kesi zao zimekuwa zikishindwa kuendelea au kwisha kinyemela wakati watoto wao wanaopata mimba au kuozeshwa wanaposhindwa kuendelea na masomo, na wengine kupata matatizo ya kisaikoloji na kiafya.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Abel Busalama, akipokea msaada huo alisema zaidi ya asilimia 30 ya watoto wakiwamo wa kike wamekuwa wakishindwa kumaliza elimu yao ya msingi na sekondari kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

# Ajali yaua dereva h'shauri, yajeruhi ofisa wa kilimo

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

DEREVA wa gari la Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Stanslaus Njau (45), amekufa huku Ofisa Kilimo wa halmashauri hiyo, Mapenzi Mshana (53), akijeruhiwa baada ya gari hilo lenye namba za usajili SM 12482 aina ya Toyota Land Cruiser kuacha njia na kupinduka.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, ACP Debora Magiligimba, alisema ajali hiyo imetokea juzi majira ya saa 21:20 usiku katika eneo la D4N Mtaa wa Mbulu, barabara ya Kahama - Isaka, Kahama Mjini.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa dereva wa gari hilo ambapo lilimshinda kulimudu na kuacha njia na kupinduka, hali iliyosababisha kifo chake na kumjeruhi ya ofisa kilimo.

"Gari lenye namba za usajili SM 12482 aina ya Toyota Land Cruiser mali ya halmashauri ya Ushetu likiendeshwa na Stanlaus Njau (45), dereva mkazi wa Mhungula likiwa linatokea Kagongwa kuelekea Kahama Mjini liliacha njia, kupinduka na kusababisha kifo kwa dereva wa gari hilo," alisema Kamanda Magiligimba.

Alisema ofisa kilimo amepata majeraha sehemu ya mguu wa kushoto.

Aliseme kuwa kwa sasa gari hilo lipo kituo cha polisi Kahama, huku majeruhi amelazwa katika Hospitali ya Halmashauri Mji wa Kahama kwa ajili ya matibabu na kwamba hali yake inaendelea nzuri, huku mwili wa marehemu umehifadhiwa hospitalini hapo ukisubiri ndugu kwa taratibu za mazishi.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akizungumza na wanafunzi wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Anderleck, iliyopo Kata ya Nyasubi, wilayani humo mkoani Shinyanga jana, wakati alipofika kukagua kama wanafunzi wanafuata taratibu za kujikinga na ugonjwa wa Covid-19. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wakulima wawezeshwa vita ya corona

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA na wadau wa kilimo wamewezeshwa vifaa saidizi vya kujikinga na maambukizo ya Covid-19 yanayosababishwa na virusi vya corona.

Uwezeshaji huo umefanywa na kampuni ya utengezezaji na usambazaji wa mbolea Yara Tanzania, ili kujikinga, huku wakiendelea na shughuli zao za kilimo.

Tukio hilo lilishuhudiwa na Katibu Tawala Msaidizi wa Kilimo na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, ambaye aliwawakilisha viongozi wengine wa Nyanda za Juu Kusini, huku akiipongeza Yara kwa kuwa mstari wa mbele katika shughuli za kilimo na hususani wakati wa janga la Covid-19.

Alitoa wito kwa mashirika mengine na watu binafsi wenye uwezo waendelee kutoa misaada na waombe maelekezo kupitia ofisi ya Mkuu wa Mkoa kabla ya kukabidhi.

"Msiogope kuja tutawapa utaratibu mzuri wa kutoa misaada hii mradi tu mje kutoa taarifa," alisema katibu huyo tawala wa mkoa.

Alisema hatua ya Yara itawapa wakulima na wadau msukumo wa kuendelea kufanya kazi za uzalishaji kwa bidii zaidi kwani wana uhakika wa kinga dhidi ya ugonjwa huu ambao hadi sasa hauna tiba.

Alisema Yara ni mdau mkubwa kwenye sekta ya kilimo na imekuwa ikishirikiana na serikali kwa karibu katika jitihada mbalimbali za kuboresha kilimo nchini.

Meneja Biashara wa Yara Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, John Rotich, alisema vifaa saidizi vilivyotolewa na kampuni hiyo ni pamoja na vitakatishi, ndoo za kunawia, huku akibainisha kuwa kampuni hiyo imetumia Sh. milioni 82 kwa vifaa hivyo katika kanda tatu nchini kwa kuanzia na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, baadaye watagawa katika Kanda ya Mashariki na hatimaye kumalizia na Kanda ya Ziwa.

Alisema wametoa msaada huo kwa wadau hao muhimu ili kuiunga serikali mkono katika vita dhidi ya corona iliyotikisa dunia na kusababisha maafa makubwa na kuporomoka kwa uchumi wa nchi nyingi kwani shughuli nyingi za uzalishaji zimesimama.

"Wakulima wanalo jukumu la kuendelea kuzalisha chakula, huku wakiendelea kujikinga ili kuepusha uwezekano wa janga la njaa kutokana na ugonjwa huu wa homa ya mapafu," alisema.

Alisema pamoja na kutoa vifaa hivyo, Yara pia itaendelea kutoa elimu kwa wakulima na wadau wengine wa kilimo kuhusu ugonjwa huu wa Covid-19 ili shughuli za kilimo ziendelee.

Baadhi ya mambo ambayo wamekuwa wakiwakumbusha wadau ni pamoja na kunawa mikono kwa kutumia sabuni na maji yakayotiririka, kupiga chafya kwa kuelekeza mdomo kwenye kiwiko, kuvaa barakoa katika sehemu zenye watu wengi na kuzingatia maelekezo ya wataalamu.

Alitoa wito kwa wanufaika wote kuhakikisha wanatumia vifaa hivyo ipasavyo na kuomba wadau wengine pia waunge mkono jitihada hizi ili iwe vita ya pamoja dhidiya Covid-19.

KWA UFUPI

## Mch. ataka tahadhari zaidi janga corona

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

ASKOFU wa Kanisa la Biblia Tanzania, Mchungaji John Mchopa, amewataka Watanzania kuendelea kuchukuwa tahadhari dhidi ya janga la corona.

Mchungaji Mchopa alisema hayo wakati akizungumza na wachungaji wa makanisa mbalimbali ya mikoa ya kusini katika ibada maalum iliyofanyika katika Kanisa la Biblia Tunduru, na kwamba viongozi wa waumini wa madhehebu ya dini wanapitia kwenye mapito magumu ambayo Mwenyezi Mungu ndiye anayejua mapito yao.

Alisema awali kutokana na kuwapo kwa ugonjwa huo, kanisa liliungana na Rais John Magufuli kuliombea taifa ili liweze kuondokana na ugonjwa huo.

Aidha, Mchungaji Mchopa alieleza kuwa viongozi hao wanaandaa utaratibu wa kugawa vifaa vya kujikinga na virusi vya corona vonavyosababisha ugonjwa wa Covid - 19.

## Wagonjwa wa nje kuhudumiwa Kilolo

**Na Francis Godwin, IRINGA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kwa kukamilisha ujenzi wa hospitali ya wilaya kwa ubora, na kuagiza kuanzia wiki ijayo kuanza kutoa huduma zake kwa wagonjwa wa nje.

"Nimeambiwa hospitali hii imeanza kutoa huduma ila kuanzia wiki ijayo ianze kutoa huduma za wagonjwa wa nje, mahitaji mengine tutaendelea kukamilisha, alisema.

Akizungumza jana wakati wa ziara yake Wilaya ya Kilolo, Jafo alisema kuwa uongozi wa halmashauri umefanya kazi kubwa na nzuri katika usimamizi wa fedha za serikali kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo na Kituo cha Afya cha Ng'uruwe.

**"Nimeambiwa hospitali hii imeanza kutoa huduma ila kuanzia wiki ijayo ianze kutoa huduma za wagonjwa wa nje, mahitaji mengine tutaendelea kukamilisha, alisema.**

# DC agawa mayai kwa wanafunzi kidato 6

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, amegawa mayai kwa wanafunzi 292 wa kidato cha sita kutoka shule za sekondari Halmashauri ya Mji wa Kahama kama moja ya kuimarisha afya zao.

Pia lengo no na kutoendelea kuwaza ugonjwa wa Covid-19 wawapo shuleni.

Wanafunzi hao wa shule za sekondari John Paul, Busoka, Mwendakulima na Anderleck, huku John Paul wakiwa wanafunzi 39, Busoka 99, Mwendakulima wanafunzi 142 na Anderleck wanafunzi 12. Macha aligawa mayai hayo kwa wanafunzi hao juzi alipokuwa na ziara ya kutembelea shule hizo kukagua namna walivyotekeleza magizo ya Wizara ya Afya namna ya kujikinga na ugonjwa wa Covid-19 kwa wanafunzi wa kidato cha sita wawapo shuleni.

Aidha, alisema kuwa lengo na kuwagawia mayai wanafunzi 292 wa kidato cha sita ni kuboresha na kuimarisha milo yao kwa kipindi hiki wawapo shuleni kwa ajili ya maandalizi ya mitihani yao ya mwisho na zoezi hili litakoma hadi pale watakapohitamu masomo yao.

"Humu wengi wenu mnaweza kumaliza masomo yenu na hamjala mayai, na hili ndio ambalo limenisukuma kuwagawia mayai kila mmoja kama moja ya kuboresha milo yenu hapa shuleni na kuimarisha afya zenu, na mtapata mayai haya mpaka pale mtakapohitimu masomo yenu ya mwisho," alisema Macha.

Hata hivyo Macha aliwataka walimu wakuu katika shule hizo kuhakikisha wanatekeleza maelekezo yalitolewa na serikali ya kila mwanafunzi kuvaa barakoa wakati awapo shuleni, ndoo za maji ya kunawia kila darasa sambamba na kukaa zaidi ya mita moja.

Pia aliwataka wanafunzi kuacha tabia ya kuazimana au kubadilishana barakoa na kuwataka kutoa taarifa kwa mwalimu pale utakapopata mabadiliko ya kimwili kama kukohoa, kupiga chafya, mafua na malaria.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mwendakulima, Neema Daniel, alisema kuwa mayai yaliyotolewa na mkuu wa wilaya yataongeza chachu ya masomo kwa wanafunzi na atahakikisha wanafunzi wote wanafanya vema kwenye mitihani yao ya mwisho.



Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha kutengeneza chaki cha Mkongoma General Supply Ltd, Geoffrey Mkongoma (kulia), akifafanua jambo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (katikati), kuhusu shughuli za uzalishaji baada ya kupelekewa nishati ya umeme, kiwandani hapo, wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani juzi. Kabla ya umeme kufika kiwanda hicho kilikuwa kinatumia Sh. milioni tano, kwa ajili ya kununua mafuta ya dizeli kwa mwezi na sasa wanatumia 400,000/- tu kwa mwezi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TFS: Bwawa la Nyerere kuwa mkombozi misitu

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umesema mradi wa bwawa la Mwalimu Julius Nyerere wa Rufiji mkoani Pwani unatarajia kuwa mkombozi katika kupunguza uharibifu wa misitu.

Uharibifu huo umekuwa ukifanywa na wananchi kwa kukata miti kwa matumizi ya kupikia pamoja na uchomaji wa mkaa.

Kamishna Mhifadhi wa Misitu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema asilimia kubwa ya uharibifu wa misitu umekuwa ukitokana na kuni na uchomaji mkaa ni kwamba uwapo wa bwawa hilo utasaidia kuibua nishati mbadala hususani gesi na hivyo kusaidia wananchi kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

"Bwawa la Mto Rufiji ni mradi wa kimkakati wa serikali, lakini sisi kama TFS tunaona kwamba ni mkombozi mkubwa kwa sababu utatusaidia na sisi kutuondolea changamoto kubwa tuliyonayo kwa wananchi kupata nishati mbadada badala ya kuendelea kutumia kuni na mkaa na kuharibu misitu yetu," alisema Prof. Silayo.

"Asilimia 92 ya Watanzania katika matumizi yao ya kila siku wanategemea nishati ya kuni au mkaa kama nishati kuu ya kupikia, kwa hiyo mradi huu utakuja kutupatia kwanza nishati mbadala ya uhakika na nafuu, lakini utapunguza utegemezi kwenye misitu."

Alisema mradi huo pia utasaidia kuibua kwa kiasi kikubwa fursa za uwekezaji katika viwanda na kuinua uchumia wa wananchi.

"Na wananchi wanapoinua uchumi wao wanapata fursa ya kuchagua aina gani ya nishati watumie, na hapo ndipo nishati ya gesi inaingia na wanaachana na mkaa, na watapata nafasi ya kuwekeza kwenye nishati ya jua kwa sababu tayari watakuwa wamejengewa uwezo," alisema Profesa Silayo.

Kadhalika, alisema TFS wamejipanga kuendelea kuwekeza katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa misitu na namna ya kuilinda.

"Katika kubadilisha watu kutoka kwenye utegemezi mkubwa wa nishati yoyote ile, ni lazima pawe na mbadala wa mabadiliko ya tabia, hulka na mtazamo. Na sisi kama TFS tutatumia fursa ya nishati mbadala kutoa elimu kwa wananchi wetu ili wabadili mitazamo yao," alisema Prof. Silayo.

# Museveni anavyoitumia corona kuahirisha uchaguzi mkuu 2021

Ukurasa 13





Ukurasa 12

## Bunge linapokoroma mifugo 'kuporwa na kuyeyuka mfugaji akishinda kesi



# Mauzauza kuelekea uchaguzi 2020

## • Nyerere aliona....

Na Magabilo Masambu

OKTOBA mwaka huu Tanzania inatarajia kufanya uchaguzi mkuu wa marais, wabunge na madiwani na hii ni kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 76(I) inayosema, "Kila baada ya bunge kuvunjwa kutakuwa na uchaguzi wa wabunge katika majimbo yote ya uchaguzi".

Ifikapo Juni 19 bunge litavunjwa na kwa mujibu wa sheria kitakachofuata ni mchakato wa kujiandaa na uchaguzi ili kutimiza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa katiba.

Mjadala wa leo unajikita kwenye mauzauza yanayojitokeza kila unapokaribia uchaguzi mkuu, ambapo sasa umekuwa kama utamaduni kwa nchi hii kwamba kila unapokaribia uchaguzi mkuu kunatokea mambo yaleyale ya miaka yote hasa kwenye eneo la baadhi ya viongozi na wanachama wa vyama mbalimbali vya siasa kuhama vyama vyao na kujiunga na vingine.

Kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 20(I) "Kila mtu anastahili kuwa huru bila ya kuathiri sheria za nchi kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika na kushirikiana na watu wengine, kutoa mawazo hadharani na hasa zaidi kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi ya wengine"Kwa hiyo si kosa kuhama chama kimoja na kwenda kingine ,wala wanaohama hawavunji sheria za nchi na taratibu zake . Ni sahihi kwa mujibu wa sheria na katiba inatamka anaweza kuhama kwaajili ya kutafuta maslahi yake binafsi au ya wengine wanahaki hiyo kikatiba hivyo hawahitaji kulaumiwa kwa kuhama kwao.

Tatizo kubwa ni sababu zinazotajwa kuwahamisha na sababu za kuhamia kwenye vyama vipya, hamahama hii limekuwa tatizo la vyama vyote vya siasa kutoka chama tawala na kutoka vyama vya upinzani.



Freeman Mbowe, kiongozi wa Chadema ambaye wabunge wamekimbia chama chake na kuendeleza siasa za kulaumiana na kutuhumiana. **PICHA : MTANDAO**

Mwaka 2015 ulishuhudia vigogo wakubwa wakitoka katika chama cha Mapinduzi(CCM) na kuhamia vyama mbalimbali kama Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na vyama vingine pia. Hawakufanya kosa kwa mujibu wa sheria na katiba tatizo ni sababu zinazowahamisha au zinazowapeleka kwenye vyama vipya.

Vilele katika uchaguzi utakaofanyika mwaka huu 2020 pia wapo ambao wameshahama hivi karibuni na pengine wapo wengi ambao wanasubiri kipenga kipigwe na kuvunjwa bunge ili wahamie na kwenye vyama vingine nao hakuna tatizo.

### LAZIMA KUTOFAUTIANA

Ni vyema kulizungumzia suala hili na wananchi na vyama ni vyema wakafahamu kuwa hakuna taasisi yoyote duniani yenye watu wenye akili timamu inaweza kuendeshwa bila kutofautiana katika mitazamo na fikra. Na hili ni jambo la kawaida na hivyo inathibitisha ubinadamu kwamba hawakuumbwa wakamilifu ndiyo maana hutofautiana kwenye kufikiri na kuamua mambo mbalimbali na hivyo hakuna siku watafanana mitazamo wala fikra.

Kwa hivyo kuhamia chama kingine kwasababu ya kutofautiana kufikiri si suluhisho la matatizo yako ambayo hayakutimizwa ulipokuwa mwanzo kwa vyovyote vile hata huko unakohamia wanatofautiana na ndiyo maana tumewaona wengine walihamia vyama fulani wakarudi kwenye vyama vyao vya zamani kwasababu pande zote wanakwenda kukutana na watu wa na si malaika.

Pili, jambo la muhimu kufahamu ni kuwa "Kusema maovu ya mtu mwingine hakukufanyi wewe kuwa mwema au kusema mapungufu ya mwingine hakukusafishi wewe na ukawa mkamilifu,hata siku moja.

Aidha, kuuelezea upungufu wako haimaanishi mimi ni mkamilifu, maana yake ni kwamba wapo wanaodhani kwamba wakisema maovu ya viongozi wao hadharani kunawafanya wao wawe wema. Hilo halipo.

Katika kitabu cha Baba wa Taifa Julius Nyerere cha Tujisahihishe, anasema "Tabia ya unafsi au ubinafsi inamfanya mtu kuficha maovu yake na kusema ya wengine".

Kusema fulani anafanya hivi na vile hakukufanyi wewe uwe mwema na hapa nieleweke vizuri sijasema maovu ya mtu yasisemwe hapana kama mtu ana maovu ambayo anayatenda kinyume cha katiba na kwa mujibu wa sheria zetu kuna vyombo vya dola. Tuna Polisi na mahakama lakini pia nadhani kuna kamati za maadili ndani ya vyama kawashitakini huko ili tuhuma za namna hiyo zishughulikiwe kisheria lakini bahati mbaya zinaishia kusemwa na kuishia hapo na jambo la ajabu ni kwamba hata wale wanaotuhumiwa hawaendi mahakamani kwa kushambuliwa.

Na wala wanaotuhumu hawaendi mahakamani kuthibitisha tuhuma mwisho wa siku uchaguzi ukipita inakuwa mwendo mdundo Wazungu wanasema 'business as usual'

Tatu kwasababu nchi yetu ni ya kidemokrasia lazima ieleweke kwamba kwenye demokrasia wachache husikilizwa na wengi huamua. Hiyo ndiyo maana halisi ya demokrasia na kwenye demokrasia hatupimi sana uzito wa hoja tunaangalia walio wengi hata kama wengi wameamua jambo la kijinga lipite ndiyo demokrasia hiyo na vilevile haimaanishi hoja za wachache kupingwa kwamba hazina mashiko hapana zinaweza kuwa na maana sana lakini kwasababu wengi wameamua basi wachache huwa inabidi waheshimu maoni ya wengi. Lakini hayo maoni ya wachache lazima yasikilizwe kwenye majadiliano ya waziwazi na wapewe nafasi ya kutetea maoni yao.

"Ni kweli kwamba demokrasia haiwezi kudumu ikiwa wachache hawatakubali matakwa ya wengi. Lakini, matakwa ya wengi hujulikana katika majadiliano au mazungumzo ya waziwazi kadhalika matakwa ya wachache hujulikana katika majadiliano na mazungumzo.

Bila wale wachache kusema waziwazi matakwa yao majadiliano hayana maana. Wakati mwingine hata baada ya majadiliano wale wachache japo wamekubali kutii uamuzi wa wengi wanaweza kuendelea kuamini kwamba mawazo yao ni sawa na ya walio wengi yamepotoka" kwa mujibu wa JK Nyerere.

***ITAENDELEA.***

***Maoni: 0689157789/0758379296***

# Bunge linapokerwa mifugo 'kuporwa na kuyeyuka



Wabunge wakiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

OPERESHENI tokomeza ujangili ya mwaka 2014 iliyosababisha vifo vya wafugaji, ukatili, kuwatesa na vipigo vya kila aina iliacha doa. Licha ya mawaziri kadhaa kuwajibika lakini wafugaji na familia zilizoathirika hazitasahau maumivu na machungu yaliyotokana na kile walichofanyiwa na vyombo vya dola.

Tasisi hizo badala ya kulinda maisha, mali na heshima ya wananchi ziliwageukia na kuwatesa, kuwadhalilisha na hata kuwaua huku mifugo nayo ikiteswa na kufa pia Suala hilo linalohusu unyanyasaji wafugaji hata sasa linazungumzwa bungeni, japo kwa utaratibu mwingine na safari hii wabunge wanahoji inakuwaje wafugaji kupoteza mifugo kwenye mikono ya dola ukiwamo mhimili wa sheria? Kwanza wanaibua madai kuwa mifugo hukamatwa kiholela, lakini pia hupotea pale mlalamikiwa anaposhinda kesi.

Ni taarifa za mifugo kukamatwa na askari wa wanyamapori bila utaratibu lakini tena wakawarudishia wanyama wao idadi pungufu wanaposhinda kesi. Jambo hili linawafanya wabunge kuwa na 'ghadhabu' na kutaka uwajibikaji zaidi.

Wanaeleza kuchukizwa na vitendo hivyo wakati wakichangia makadirio na matumizi ya Wizara ya Uvuvi na Mifugo kwenye mkutano unaoendelea mjini Dodoma.

Baadhi ya wabunge wanaitaka serikali kuwa na utaratibu maalumu wa kutatua changamoto hiyo, kwani umekuwa ukiwakandamiza wafugaji kwa muda mrefu.

Wabunge wao walisema askari wanyamapori wamekuwa wakikamata mifugo ya wafugaji na kuwadhurumu pindi mifugo inapoingia katika hifadhi. Mbunge wa Simanjiro (CCM), James Ole Millya, anaitaka serikali kushughulikia matatizo ya wafugaji kwani wengi wamekuwa wakinyang'anywa mifugo yao na askari wanyamapori.

Anasema hata inapotokea wafugaji wanaporudishiwa mifugo yao wakishinda kesi, hupewa pungufu ikilinganishwa na idadi kamili iliyokamatwa, akisema kumekuwa na uonevu mkubwa wa uporaji wa mifugo unaofanywa na mamlaka za serikali, akitaja kuwa mfugaji anaporwa mifugo 300 baada ya miaka mitatu kesi kuisha anarudishiwa ng'ombe 100.

> "Majukumu ya DPP yapo kikatiba na hayaingiliwi na mtu yeyote, anapokata rufani anakuwa na sababu ya kufanya hivyo, inawezekana kuna kutafsiriwa vibaya kwa sheria.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina , akijibu hoja na kutoa ufafanuzi bungeni.

Martha Umbulla (viti maalumu CCM), anazungumzia malalamiko mengi ya wafugaji ambayo yamedumu kwa muda mrefu anayosema yanapaswa kusikilizwa na kutatuliwa.

"Kilio hicho sio cha leo, mimi ninatoka katika jamii ya wafugaji malalamiko haya ni ya kweli ifike mahali yaangaliwe, kwa kufanya hivyo itaweza kuweka utulivu kwa wafugaji. Wafugaji wanamshukuru Rais John Magufuli kwa kuunda timu ya kutatua migogoro lakini ni lazima itatuliwe kwa wakati."

Wabunge wengine wanaochangia mjadala wa wafugaji kuonewa ni Edwin Sanda (CCM), Kondoa Mjini, anayesema: "Hivi kuna tatizo gani ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP)? Wafugaji wamekuwa wakishinda kesi lakini hawarudishiwi mifugo?Anashinda ofisini na kuagiza mawakili kukataa rufaa, hiyo siyo sawa".

Mbunge wa Monduli (CCM), Julius Kalanga, anasema:"Hivi ni kwa nini wafugaji wasipewe mifugo yao wanaposhinda kesi?, Ng'ombe wanakamatwa wengi lakini wanarudishiwa wachache kwa kisingizio kuwa wamekufa".

Wakati wabunge wakiwatetea wafugaji na kutaka serikali kuchukua hatua, Sixtus Mapunda, Mbinga Mjini (CCM), anaipongeza wizara hiyo kwa kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji nchini, akitaka kuwekwe utaratibu wa kuwatengea maeneo wafugaji ili waondokane na mazoea ya kuingiza mifugo katika mbunga za wanyama.

"Wafugaji hawana shida, wanaingia katika maeneo wakati wa kipindi ambacho hakuna nyasi, lakini ng'ombe anakula nyasi hali miti kwa nini tusitengeneze utaratibu maalumu wa kuingiza ng'ombe katika hifadhi ili walete mbolea?,"anasema Mapunda

### MWANASHERIA MKUU

Malalamiko yao yanamlazimisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Profesa Adelardus Kilangi, kusimama na kutolea ufafanuzi, akijibu hoja za wabunge anasema ukamataji wa mifugo inayoingia katika hifadhi za wanyama unafanyika kwa mujibu wa sheria ambayo ilitungwa na wabunge wenyewe.

Anasema hakuna wafugaji ambao wananyang'anywa mifugo yao kwa uonevu na kwamba ni kinyume cha sheria mifugo kuingia katika hifadhi za taifa. Profesa Kilangi anaendelea kufafanua kuwa ni kweli utekelezaji wa sheria hiyo unachangamoto lakini serikali inaendelea kuzitatua.

Kuhusu mifugo kuendelea kushikiliwa baada ya kesi kumalizika, Kilangi analiambia bunge kuwa mahakama inapotoa hukumu na mifugo kuendelea kushikiliwa kunaweza kuwa na tatizo sehemu fulani, hivyo serikali itafuatilia kwenye kesi zote ili kufahamu ni kesi gani ambazo zimeshatolewa hukumu lakini mifugo bado inaendelea kuzuiliwa.

Kuhusu Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kukata rufani mfugaji anaposhinda kesi mwanasheria mkuu wa serikali anasema: "Majukumu ya DPP yapo kikatiba na hayaingiliwi na mtu yeyote, anapokata rufani anakuwa na sababu ya kufanya hivyo, inawezekana kuna kutafsiriwa vibaya kwa sheria".

Luhaga Mpina, Waziri wa Uvuvi na Mifugo, anasema kwenye mifugo wizara imetunga kanuni 20 ambazo zinataleta mageuzi ya kweli kwa wafugaji.

Anaeleza kuwa kuna baadhi ya kanuni iliyotungwa ya mifugo ambayo italinda mifugo kutopata magonjwa na pia kanuni hizo zinakwenda kuleta mageuzi katika sekta ya uvuvi ambapo wataweza kupata neema na mageuzi makubwa.

### KUKAMATA MIFUGO

Kuhusu mifugo kukamatwa, Waziri Mpina anasema wanaendelea kutatua changamoto hizo na kwamba aliwahakikishia wafugaji wataendelea kupata haki zao.

"Hii bajeti ninayoisoma leo ni ya tatu bungeni, awali nilipokuwa nasoma nilikuwa napata changamoto nyingi kutoka kwa wabunge kwa sababu matatizo na kero zilikuwa nyingi, lakini leo napigiwa makofi, ni manufaa makubwa na mageuzi tuliyoyaleta," anasema Mpina.

Kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji, Waziri anaeleza kuwa ipo lakini inahitaji tathimini kubwa katika kuitatua na kwamba wizara imeshaifanyia upembuzi na tathmini kuhusu migogoro hiyo na kwamba baadhi yameanza kuitatua ikiwamo migogoro mikubwa 11 kati ya 17.

Anasema imetatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji ambayo awali ilikuwa inasababisha vita miongoni mwao na sasa kuna amani tele.

# Museveni anavyoitumia corona kuahirisha uchaguzi mkuu 2021

**Na Mashaka Mgeta**

FEBRUARI mwakani, Uganda inatarajiwa kufanya uchaguzi mkuu, utakaomuwezesha Rais Yoweri Museveni, kuingia madarakani kwa muhula mwingine tena.

Kiongozi huyo kwa mara ya kwanza aliingia ikulu mwaka 1986 na hadi sasa kuongoza taifa hilo kwa miaka 34.

Kinara huyo wa utawala katika ukanda wa Afrika Mashariki, anatarajiwa kupambana na wagombea wengine, wakiwamo 24 ambao kabla ya kusimamishwa kwa shughuli za kijamii ikiwemo mikutano ya kisiasa kutokana na maambukizo ya virusi vya corona, walishaanza kutimiza masharti ili kuwania kiti hicho.

Lakini kwa hali ilivyo sasa, ni kama matumaini kwa Waganda kushiriki uchaguzi mkuu huo yanaendelea kupotea kutokana na tamko la Rais Museveni na washirika wake kutaka kuahirishwa kwa uchaguzi huo wa Februari mwakani. Mwanzoni mwa mwezi uliopita, alifungua' mjadala huo kupitia kauli yake kuwa uchaguzi mkuu nchini humo ungeweza kusogezwa mbele endapo maambukizo ya corona hayatadhibitiwa.

Museveni alikaririwa akihojiwa na kituo cha runinga cha NBS akisema, "itakuwa hatua ya wendawazimu kuuandaa wakati kuna janga la virusi vya corona."

Rais wa Uganda akasema ikiwa maambukizo ya virusi vya corona hayadhibitiwa kufikia Julai, mwaka huu, itakuwapo haja ya kutathmini upya mchakato wa uchaguzi huo.

**WAGOMBEA LUKUKI**

Wakati hayo yakijiri, rekodi inaonyesha kuwa kiasi cha wagombea 24 wameshatangaza nia ya kuwania urais nchini Uganda, kila mmoja akijinasibu kutaka kumuengua madarakani 'nguli' huyo wa utawala katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Wagombea hao walishaanza kukutana na wafuasi wao kwenye ngazi za matawi, kabla ya kuibuka kwa maambukizo ya corona, ikiwa ni sehemu ya kujitayarisha kwa uteuzi kama inavyotakiwa na Tume ya Uchaguzi ya nchi hiyo.

Mbunge wa Kyanondo Mashariki, Robert Kyagulanyi, maarufu kama Bobi Wine, anayedaiwa kugusa hisia za wapiga kura wengi hasa vijana, ni miongoni mwa waliotangaza kuwania urais dhidi ya Museveni.

Hata hivyo, hatua ya kutangaza nia kwa wagombea hao inahusishwa na kadhia za kisiasa zinazowakabili, ikiwamo kukamatwa na polisi, kuwekwa ndani na kufunguliwa kesi mahakamani.

Mathalani, Bobi Wine amewahi kupitia hatua hizo na hatimaye kufunguliwa mashtaka ya kupanga njama za kuipindua serikali ya Rais Museveni.

Mwanasiasa mwingine, Jenerali Henry Tumukunde, aliyewahi kuwa Waziri wa Usalama na mshirika wa karibu wa Rais Museveni, naye alikutwa na kadhia kama hizo kwa kuwekwa ndani kwa takribani miezi miwili, kisha kufunguliwa kesi yenye mashtaka ya kupanga njama za kuipindua serikali.



Museveni na Kainerugaba (kulia), anayedaiwa kumuandaa awe mrithi wake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Chama chake cha National Resistance Movement (NRM) kilitawala Uganda kama taifa la chama kimoja hadi kura ya maamuzi ilipofanyika 2005 na kurejesha mfumo wa vyama vingi.



Bobi Wine, mwanamuziki na mwanasiasa matata nchini Uganda, aliyetangaza kugombea urais mwakani.

Matukio yanayowasibu wanasiasa hao yanatolewa ufafanuzi mfupi na Rais Museveni, anapokaririwa akisema kadhia hizo zinawakuta watu wanaochanganya siasa na njama za kutaka kupindua utawala wake. Ingawa haihusishwi na kauli hiyo, lakini kumezidi kuwepo hisia na hofu ya muda mrefu nchini humo kama uchaguzi mkuu huo utakuwa wa haki na huru, miongoni mwa sababu zinazotajwa ni matukio ya vitisho na unyanyasaji dhidi ya wapinzani.

Lakini taarifa zaidi zinaeleza kuwa kuahirishwa kwa uchaguzi huo kadri ya maelezo ya Rais Museveni, kunaifanya hatima yake kuwa mikononi mwa wanasayansi watakaoamua lini utafanyika.

Lakini suala hilo linapokelewa kwa hisia tofauti nchini humo. Kama ilivyotarajiwa, walio wengi katika upinzani nchini wamepinga na kumkosoa Rais Museveni, na wengine wakaenda mbele zaidi kudai kwamba anataka kutumia COVID -19 kung'ang'ania madarakani.

Lakini kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali ikiwamo kituo cha habari cha Ujerumani (DW), Rais Museveni anawaamini wanasayansi kwa vile ushauri wao kwake, umechangia kuifanya nchi hiyo kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona kwa kiasi kikubwa.

Ni kutokana na hoja hiyo, Rais Museveni anaendelea kuwategemea wanasayansi kutoa ushauri kuhusu muda muafaka wa kufanyika kampeni na uchaguzi mkuu.

Hoja hiyo inawagusa wengi na kuibuliwa katika kongamano la vyama vya kisiasa ambapo washiriki wanaomuunga mkono kiongozi huyo walikitetea kuwa ni halali na kwamba uchaguzi huo unapaswa kuahirishwa kwa mwaka mmoja ama miwili, huku wanaompinga wakiendelea kumkosoa.

Miongoni mwa wanaompinga ni mbunge wa Bugiri, Asuman Basalirwa, anayesema, pamoja na ukweli wa nchi hiyo kukabiliwa na corona kama ilivyo kwa mataifa mengine, lakini katiba ya Uganda lazima ifuatwe huku wanasayansi wakipewa fursa ya ushauri kuhusu namna bora ya kufanikisha kampeni na uchaguzi bila kusababisha maambukizo.

Naye Rais wa chama cha Forum for Democratic Change (FDC), Patrick Okoboi, anasema ili nchi ifikie hatua ya kuahirisha uchaguzi mkuu kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo, ni lazima kuwapo tukio lililosababisha kutangazwa kwa hali ya hatari, lakini Uganda haijafikia hatua hiyo kwa sababu ya corona.

Awali, mjadala kuhusu kuahirishwa kwa uchaguzi huo uliegemezwa zaidi katika sababu za kiuchumi, kwamba taifa hilo lingeweza kuyumba katika nyanja hiyo kutokana na mfululizo wa mambo ambayo, miongoni mwa mambo mengine, yangewasababisha wawekezaji na wajasiriamali kupunguza ama kutoweka mitaji yao kwenye uwekezaji.

Mwaka 2016, shirika la habari la Uingereza (BBC) liliwahi kuripoti kuwa Museveni alisifiwa kwa kuimarisha uthabiti kisiasa na ukuaji wa uchumi nchini humo, baada ya miaka mingi ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na ukandamizaji wa wapinzani chini ya watangulizi wake Milton Obote na Idi Amin.

Shirika hilo likamtaja Museveni kama mmoja wa waasisi wa kundi mojawapo la waliosaidia wanajeshi wa Tanzania kuliomuondoa madarakani Idi Amin mwaka 1979.

Baadaye, Museveni aliunda jeshi ljipya la waasi ambalo lilifanikiwa kutwaa uongozi 1986.

Chama chake cha National Resistance Movement (NRM) kilitawala Uganda kama taifa la chama kimoja hadi kura ya maamuzi ilipofanyika 2005 na kurejesha mfumo wa vyama vingi.

**KUMRITHISHA MTOTO**

Licha ya maelezo mengi kuna uvumi kwamba Museveni anamtayarisha mwanawe Muhoozi Kainerugaba, kuwa mrithi wake.

Museveni alizaliwa magharibi mwa Uganda mwaka 1944, akasomea sayansi ya siasaTanzania na alipigana pamoja na wapiganaji wa Front for the Liberation of Mozambique (Frelimo), ambapo alipata ujuzi wa vita vya msituni.

***MITANDAO***

***Maoni- 0754 691540***

# Mbunge aliyebadili gia angani alivyoibuka na kuja kivingine



Lwakatare katika mikutano ya ya chama chake cha zamani kabla ya kuikimbia Chadema. **PICHA: AFP**

**Na Sabato Kasika**

‘UKISEMA cha nini, wenzio wanasema watakipata lini’. Hivyo ndivyo inaweza kuwa imetokea kwenye anga za siasa nchini baada ya mbunge wa Bukoba Mjini, Wilfred Lwakatare, kurudi nyumbani CUF.

Huyo ni miongoni mwa wabunge waliofukuzwa katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) baada ya kukaidi maelekezo ya chama ya kutohudhuria vikao vya bunge kwa siku 14.

Lengo la chama kutoa maelekezo hayo kwa wabunge wake lilikuwa ni kukaa karantini kwa siku hizo ili kujiepusha na maambukizo ya corona ambavyo inasumbua dunia licha ya kwamba kwa Tanzania tatizo linaelekea kupungua.

Baada ya kukaidi maelekezo hayo, Chadema iliwafukuza uanachama na Lwakatare ameamua kujiunga na CUF uamuzi, unaoweza kuchangiwa na chama kumtimua.

Mbunge huyo anarudi CUF huku tayari akiwa ametangaza kutowania ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu na pia kutojishughulisha na siasa na badala yake amejipanga kufanya shughuli zake nyingine.

Huenda inawezekana kitendo cha kumfukuza ndicho kilichosababisha hayo, kwani Waswahili wanasema; ‘ukisema cha nini, wenzio wanasema watakipata lini’.

Chadema imemfukuza Lwakatare na kumbe CUF bado inamhitaji, hivyo uamuzi huo wa kumtosa umechangia kumfanya mwanasiasa huyo abadili ‘gia angani’ na kuendelea na siasa kama kawaida.

**KUSTAAFU**

Lwakatare ni miongoni mwa wabunge ambao waliwahi kutangaza kuachana na siasa ikiwamo kutowania ubunge katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

> “Lwakatare hakurudi CUF kwa ajili ya kutafuta cheo, bali anarejea nyumbani kwa mapenzi kwa chama hicho, lakini pia lengo la CUF ni kuhakikisha vyama vya upinzani vinashinda.



Mbunge Lwakatare baada ya kurudi rasmi CUF, chama anachojinasibu kukiasisi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Hivi karibuni akiwa bungeni jijini Dodoma, Lwakatare aliwaaga wabunge wenzake na kusema hana mpango wa kugombea ubunge katika uchaguzi mkuu na anastaafu siasa.

Lakini Mei 30 mwaka huu alirudi katika chama cha CUF na kupokelewa na Makamu Mwenyekiti wa CUF Bara, Maftah Nachuma, kwenye makao makuu ya chama hicho yaliyopo Buguruni Dar es Salaam.

Katika mapokezi hayo, mwanasiasa huyo alitoa sababu za kwenda kinyume na msimamo wake wa kustaafu siasa kwamba; CUF ilimuomba arudi nyumbani, hivyo hakuona sababu za kukataa.

“Miaka mitatu, nilitangaza wazi hata bungeni wanafahamu nikasema natarajia ifikapo Oktoba 2020 nikimaliza kipindi cha bunge sigombei tena nataka nipumzike ili nifanye mambo mengine. Mungu ana muda wake. Nimebakiza mita chache kumaliza mbio nashtukia leo nimeinuliwa tena,” anasema Lwakatare.

**CUF KUMTUMIA**

Mbunge huyo wa Bukoba Mjini anasema, yeye ni miongoni mwa watu waliokiasisi chama cha CUF, hivyo amerudi ili kuhakikisha kinaimarika, hususan kuelekea uchaguzi mkuu Oktoba 2020.

Chama hicho kinakiri Lwakatare alikimaliza kanda ya ziwa alipojiunga na Chadema na sasa kitamtumia kuimaliza vyama vya Chadema na CCM, ACT-Wazalendo kwenye kanda hiyo kwani ni mwiba kwa vyama hivyo.

Nachuma anasema, CUF itamtumia Lwakatare kuvimaliza vyama vya upinzani hasa Chadema katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu na kwamba ni kama CUF imezaliwa upya.

“Lwakatare hakurudi CUF kwa ajili ya kutafuta cheo, bali anarejea nyumbani kwa mapenzi kwa chama hicho, lakini pia lengo la CUF ni kuhakikisha vyama vya upinzani vinashinda,” anasema Nachuma.

**VYAMA KICHEKO**

Kila mwaka wa uchaguzi mkuu, huwa ni wakati wa vyama vya siasa kuvuna wanachama wapya wakiwamo pia wa zamani wanaoamua kurudi katika vyama vyao vya zamani.

Tayari baadhi vimeshaanza kuvuna wanachama vikiwamo vya CCM, NCCR- Mageuzi na CUF ambacho kimempokea mwanachama wake wa zamani Lwakatare aliyemua kuendelea na siasa.

Kwa upande wa CCM, kilishapokea wabunge na madiwani wengi kutoka upinzani na wapo wengine wanaoomba kujiunga akiwamo mbunge wa Kilombero Morogoro, Peter Lijualikali kutoka Chadema.

Mbunge huyu kijana ni miongoni mwa wabunge waliofukuzwa katika chama hicho akituhumiwa kwa makosa kama ya Lwakatare. Pamoja nao ni Joseph Selasini jimbo la Rombo na Anthony Komu akiwakilisha jimbo la Moshi Vijijini na wote wametangaza nia ya kurudi NCCR-Mageuzi.

**WANASIASA HAWAAMINIKI?**

Kuwapo na dhana kwamba wanasiasa hawaaminiki, hawana msimamo, eti wakati wowote wanaweza kubadilika, si watu wa kusimamia kile wanachokisema, hivyo kuwaamini ni kujiumiza.

Sina uhakika na dhana hiyo iwapo ina ukweli ndani bali ninachotambua ni kwamba kila mmoja ana haki na kujiunga au kuhama cha siasa ili mradi amekidhi vigezo vilivyowekwa na chama anachohamia.

Lakini, pia muhimu wanasiasa kuzingatia itikadi na imani za vyama vyao kuliko kila kukicha kuhama chama hiki kwenda kile, hali ambayo wakati inaweza kutafsiriwa kwamba hawana msimamo.

Hii inatokana na ukweli kwamba chama cha siasa ni itikadi na ndiyo inayozaa imani, hivyo suala la kuhama chama la kufanya ghafla kama kweli mwanachama ameingiwa na imani ya chama chake.

Sidhani kwamba ni rahisi kubadili imani kirahisi, vinginevyo mwanachama awe mtu asiyeamini katika itikadi na imani chama au labda hakina itikadi au imani ambayo wanachama wanatakiwa kufuata.



## RC awapa jukumu ma-DC wananchi kujiunga na CHF

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuwahamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulioboreshwa ili kupata matibabu kwa gharama nafuu.

Agizo hilo alilitoa juzi alipozungumza kwa nyakati tofauti na wananchi kwenye mikutano mbalimbali ya kuhamasisha shughuli za maendeleo katika mkoa huo.

Dk. Mahenge aliwaagiza wakuu wa wilaya wote na wakurungenzi wa halmashauri zote kuhakikisha wanawahamasisha wananchi kujiunga na mfuko huo wa bima ya afya, ili kuwasaidia kupunguza gharama wakati wa matibabu.

"Mwaka huu mvua imenyesha vizuri, hivyo tunatarajia wananchi kuvuna mazao ya kutosha ya chakula na biashara, ninawaagiza kila mkuu wa wilaya na wakurugenzi wahakikishe kipindi hiki cha mavuno anaihamasisha jamii kujiunga na bima ya CHF," aliagiza.

Mkuu wa Mkoa huyo pia aliagiza uhamasishaji huo ufanyike kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji hadi wilaya na uhamasishaji ufanyike kwa kila kaya.

Aliwataka wahakikishe wanazihamasisha kaya zote ambazo hazijahuisha uanachama wao, zifikiwe ili walipe ada ya CHF kwa ajili ya gharama za matibabu.

Vilevile, Dk. Mahenge aliwaagiza waganga wakuu wa wilaya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama, ili kutoa ushuhuda kwa wananchi ambao hawajajiunga na mfuko huo.

"Mhakikishe mnawasilisha mapema na kwa wakati madai yote kupitia mfumo wa kieletroniki na fedha zinazolipwa kwenye vituo zitumike kulingana na mwongozo," aliagiza.

Mratibu wa Mfuko wa CHF mkoani Dodoma, Dk. Francis Lutalala, alisema kwama, hadi kufikia Aprili 30 mwaka huu, kaya 47,141 zenye wanaufaika 282,846, zilikuwa zimeandikishwa kwenye mfuko huo.

Dk. Lutalala alisema kwa sasa CHF inatekelezwa nchi nzima na wananchi wanatakiwa kuchangia kiwango cha Sh. 30,000 kwa kaya yenye watu sita kwa mwaka mzima, ikiwa ni sawa na kila mwanafamilia kuchangia Sh. 5000 tu kwa mwaka.

Alitoa takwimu za kila wilaya zilivyoandikisha hadi kipindi hicho alichokitaja kuwa Bahi kaya 3,758, Chamwino 4,939, Chemba 1,102, Dodoma 6,292 na Halmashauri ya Kondoa 1,804.

Aliendelea kutaja wilaya zingine kuwa ni Mpwapwa kaya 6,367, Kondoa Mji 694 na Kongwa 5,802 na kwamba wanaendelea kuhamasisha wananchi wengine kujiunga na mfuko huo.

Dk. Lutalala alisema hadi kufikia kipindi hicho, CHF imelipa zaidi ya Sh. milioni 496.8 kwa vituo vya huduma za afya 330 vilivyotibu wanachama na kuwasilisha madai kwao.

"Moja ya vipaumbele vya serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wengi zaidi wanapata matibabu bora bila usumbufu," alisema.

# Waziri aona fursa mafuta ya kula

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, ametaka Watanzania kuwekeza katika sekta ya mafuta ya kula kutokana na kuwapo soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Alitoa rai hiyo juzi alipotembelea na kukagua kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula cha Sunshine kinachozalisha mafuta yanayotengenezwa kwa kutumia malighafi ya alizeti yanayoitwa Sunbelt kilichoko katika eneo la Zuzu jijini hapa.

Alisema ni vyema Watanzania wakaendelea kuchangamkia fursa ya kilimo cha zao la alizeti kwa kuzingatia uhitaji mkubwa wa mafuta ya kula nchini kwani nchi imekuwa ikipoteza zaidi ya Sh. bilioni 443 kwa mwaka kwa kuagiza mafuta nje ya nchi.

Waziri huyo alibainisha kuwa uwekezaji huo ni miongoni mwa fursa muhimu na kuwataka wenye uwezo kulima zao hilo kwa wingi, kuchangamkia fursa hiyo kwa vile zao hilo linastawi katika ukanda huo.

Waziri Kairuki alipongeza uwekezaji katika kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha tani 25 kwa siku na kilichowekeza zaidi ya Sh. bilioni 230.

"Niwapongeze kwa uwekezaji mkubwa mlioufanya katika eneo hili tangu mwaka 2015 na hii inaleta chachu kwa wawekezaji wazawa kuona fursa na soko la malighafi wanazozalisha hasa zao la alizeti," alisifu.

Waziri Kairuki aliwataka wataalamu wa masuala ya kilimo kutoa elimu kwa umma kuhusu kilimo bora cha zao hilo ili kuwa na utaalamu wa kutosha na kutumia mbinu za kisasa na zenye kuzingatia viwango vinavyotakiwa.

Awali, akitoa taarifa ya kiwanda hicho, Meneja Biashara na Maendeleo wa Kiwanda hicho, Krishna Urs, alieleza wanayokabiliana uhaba wa malighafi kwa ajili ya uzalishaji.

Alitoa wito kwa wadau kuitumia fursa ya kilimo cha zao hilo ili kuendana na mahitaji halisi.

"Ni muhimu kuwekeza zaidi katika alizeti kwa sababu soko lake lipo na hii itatatua changamoto ya kuzalisha kwa uchache na kuwafikia wananchi wengi na kupata soko la nchi za nje," alisema Krishna.

Ofisa Viwango wa Kiwanda hicho, Upendo Mganda, alisema uwekezaji huo umesaidia kutoa ajira na vibarua kwa wananchi walio wengi.

"Tunashukuru uwapo wa kiwanda umetusaidia kupata ajira na wazawa wameweza kuuza malighafi zao kiwandani hapa kwa bei yenye tija," alisema.

Upendo alisema ni kiwanda chenye tija kwa kuzingatia uwezo wake wa uzalisha tani 24 hadi 25 kwa siku na kinafanya vizuri sokoni kwa kuzingatia kuwa mafuta yanayozalishwa hayana kemikali zenye athari kwa watumiaji.

"Uzalishaji ni wa kuridhisha japo kuna vikwazo ya uchache wa malighafi unaochangia kusuasua kwa uzalishaji na kusababisha kuzalisha kwa msimu, hivyo kutolifikia mahitaji halisi nchini," alisema.



Kamishna Jenerali wa Magereza, Suleiman Mzee, akipiga makofi huku akiwa ndani ya moja kati ya malori matatu mapya aina ya TATA yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 400, aliyoyakabidhi kwa kikosi cha ujenzi cha shirika la uzalishaji mali la Magereza (SHIMA), jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Magereza wapewa magari ya mamilioni

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KAMISHNA Jenerali wa Jeshi la Magereza, Suleiman Mzee, amekabidhi magari matatu yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 400 kwa ajili ya kusaidia kwenye miradi mbalimbali ya ujenzi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza (Shima).

Jeshi hilo kwa muda mrefu limekuwa likikodisha magari kwa ajili ya kubeba mchanga, hivyo kwa sasa wamepunguza gharama na watanunua mafuta kwa kuwa magari wanayo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Kamishna Mzee alisema jeshi limejipanga kugawa magari hayo kwa magereza yote nchini, lakini kipaumbele kitatolewa kwanza kwa magereza 20 ya uzalishaji.

Alisema magari hayo yamesaidia kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho hakukitaja, lakini akasema watafanya tathmini kujua walikuwa wakitumia kiasi gani cha fedha ambacho hivi sasa wamefanikiwa kukiokoa.

"Nimekabidhi Shirika la Magereza ninaomba mkayafanyie kazi ipasavyo, magari haya yakatumike kwenye shughuli za ujenzi ambazo tulipata shida kwa kukodi magari," alisema.

Alisema lengo kwa sasa ni kuona watu wanafanya kazi na si kulegalega wakati vifaa vyote wanavyo.

Alibainisha kuwa mpango huo si kwa Gereza la Isanga pekee, bali ni kwa magereza yote nchini ambayo yapo zaidi ya 120.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa jeshi hilo, Chacha Bina, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shima, alishukuru kwa kukabidhiwa magari hayo, akibainisha kuwa yatawasaidia katika kurahisisha kazi za ujenzi ikiwamo kupunguza gharama ya kukodi magari ya mchanga.

"Ninamshukuru Kamishna tangu ameingia kwenye jeshi hili mambo mengi yamebadilika," Kamishna Bina alisifu.

Alisema shirika litafanya kazi kwa bidii kuhakikisha linayatumia vizuri magari hayo kwa ajili ya kukamilisha shughuli za ujenzi wa taifa.

Alisema kilio chao kilikuwa kupata magari na sasa wamepata, hivyo kazi zao watazifanya kirahisi tofauti na mwanzo ilipokuwa inawawia ugumu kufanya kazi za ujenzi za shirika hilo.



## CCM yatekeleza ahadi ujenzi wa shule za Kyela

**Na Grace Mwakalinga, KYELA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Kyela, kimetimiza ahadi ya mifuko 60 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Msingi Nkuyu na Shule ya Sekondari Nyasa Lakeshore ikiwa ni sehemu ya kutekeleza ilani yake ya uchaguzi.

Akikabidhi mifuko hiyo juzi, Katibu wa CCM Wilaya, Lucas Nyanda, alisema ahadi hiyo ni sehemu ya kutekeleza wajibu wa kuwatumikia wananchi na kukidhi mahitaji kama maelekezo ya ilani ya uchaguzi yanataka.

Alisema waliahidi na kukamilisha ahadi yao mwisho mwa mwezi Mei na walifanya hivyo lakini mifuko mingine ya saruji ili kusaidia ukarabati wa Shule ya Msingi Nkuyu ambayo majengo yake yamechakaa na kuhatarisha usalama.

"Moja ya majukumu ya chama cha mapinduzi ni kuboresha huduma za kijamii ikiwamo shule na hospitali, mambo mengi mazuri ambayo tunapaswa kujivunia, lakini hatujafanya pekee yetu bali kwa kushirikiana na serikali, Shule ya Msingi Nkuyu ni miongoni mwa shule kongwe wilayani Kyela, lakini haijawahi kufanyiwa ukarabati licha ya kubeba wanafunzi wengi ambao ni zaidi ya 500 hakuna madarasa ya kutosha na yaliyopo yamechakaa tuliahidi mifuko ya saruji na tumetimiza, mahitaji bado yapo tutajitahidi kutoa tena," alisema Nyanda.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Hunter Mwakifuna, alisema chama kwa kushirikiana na Kampuni ya Bioland wamekuwa mstari wa mbele kuboresha miundombinu ya shule mbalimbali wilayani humo.

Alisema ni Kampuni ya Bioland na mshirika wake Kim's Chocolate ambayo inajihusisha na ununuzi wa kakao imekuwa ikijenga shule nyingi kwa kutumia faida wanayoipata ambapo hadi sasa jumla ya madarasa 800 yamejengwa na kampuni hiyo.

Diwani wa Matema, Issa Solomon, alikipongeza chama kwa msaada huo na kusema ukarabati wa majengo hayo ukikamilika utasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu.

Naye Katibu Mwenezi wa CCM, Emmanuel Mwamlinge, aliwataka wananchi kuzidi kukiamini chama hicho kwa madai kuwa kipo kwa lengo la kutatua matatizo mbalimbali yanayowakabili ikiwapo kuwasogezea huduma za kijamii karibu.

**Alisema ni Kampuni ya Bioland na mshirika wake Kim's Chocolate ambayo inajihusisha na ununuzi wa kakao imekuwa ikijenga shule nyingi kwa kutumia faida wanayoipata ambapo hadi sasa jumla ya madarasa 800 yamejengwa na kampuni hiyo.**

# Watakaowapa wanafunzi hofu ya corona waonywa

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amepiga marufuku mtu yeyote atakayetoa vitisho dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 kwa wanafunzi wa kidato cha sita na vyuo.

Wanafunzi hao ni waliorejea masomoni Jumatatu, badala yake wawakumbushe kuendelea kuchukua tahadhari.

Waziri Jafo alitoa kauli hiyo jana akiwa mkoani Mbeya na kufanya ziara ya kushtukiza kwenye Shule ya Sekondari ya Mbeya Day kwa lengo la kuangalia mahudhurio ya wanafunzi siku ya kwanza tangu shule zifunguliwe.

Alisema wakati huu shule zimefunguliwa ni nafasi kwa wanafunzi wa kidato cha sita waendelee kujiandaa na mitihani ya kuhitimu badala ya kusikia vitisho juu ya ugonjwa wa Covid-19.

"Kusiwapo kwa vitisho dhidi ya wanafunzi kuhusu ugonjwa huo wa corona hasa wa kidato cha sita waachwe wajiandae vema na mitihani yao ya kitaifa," alisema Waziri Jafo.

Alieleza kufurahishwa na idadi ya wanafunzi 180 kuripoti shule na kuanza masomo Shule ya Sekondari Mbeya Day na kuwakumbusha kuendelea kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya, huku walimu wakitoa mwongozo namna ya kuishi shuleni hapo.

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo aliagiza Halmashauri ya Jiji la Mbeya kununua vifaa vyote vya kukamilisha ukarabati wa Shule ya Sekondari Mbeya Day ili wanafunzi wengine watakaporuhusiwa kuanza masomo wakute kazi hiyo imemalizika.

"Baadaye tutarajia wanafunzi wengine kurudi shule kwa kadri maelekezo yatakavyotolewa, hivyo ni muhimu ukarabati wa majengo yote kukamilika ili kuepusha usumbufu," alisema.

Awali akisoma risala ya ukarabati wa shule hiyo, Mwalimu wa Shule hiyo, Julius Kalinga, alisema kazi ya ukarabati inafanywa na Jeshi la Kujenga Taifa JKT cha Itende na ununuzi wa vifaa vya ujenzi unafanywa na Halmashauri ya Jiji.

Alisema vifaa vyote vipo na ukarabati wa majengo hayo unazingatia vigezo vya ubora na kumwahidi Waziri Jafo kukamilika kwa wakati.

Fundi Mkuu wa Kikosi cha Itende JKT, Alfred Ngonyani, alisema wanatarajia kukamilisha kazi ya ukarabati wa shule hiyo Juni 16, mwaka huu endapo hakutakuwa na uhaba wa vifaa vya ujenzi.



Mwenyekiti wa Machifu wa Jiji la Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga (mwenye shuka jeupe), akizungumza na waandishi wa habari jijini humo jana, kuhusu historia ya jengo la ofisi ya zamani ya Mkuu wa Mkoa, ambalo limevunjwa ili kupisha ujenzi wa majengo mapya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Inyala waja juu nyumba kubomolewa bila fidia

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ZAIDI ya wakazi 40 wa Kijiji cha Inyala, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuingilia kati suala la kutakiwa kubomoa nyumba zao wenyewe bila fidia.

Wakazi hao wameamriwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini, (Tarura) ili kupisha ujenzi wa barabara ya Inyala-Simambwe ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami.

Wakizungumza na Nipashe kijijini hapo jana walisema Tarura inawalazimisha kubomoa nyumba zao bila fidia, huku wakiwatolea vitisho hali ambayo inasababisha waishi kwa hofu na hivyo wanaomba serikali iingilie kati ili waweze kutendewa haki.

Mmoja wa wakazi hao, Antony Luba, alisema waliambiwa wabomoe wenyewe kabla wao hawajaanza zoezi hilo na kwamba kila wakigomea watalipa fedha zaidi ya Sh. 500,000.


"Tulijitahidi kuongea na viongozi mbalimbali wa vijiji na kata, lakini hawakuchukua hatua yoyote wala kutupa majibu ya kuridhisha tumebaki na maswali mengi licha ya kuwa tunaamini serikali yetu ni sikivu," alisema Luba.

Naye Marisela Majanga, alisema maeneo hayo wanayatumia kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwamo makazi, kilimo na biashara hivyo waliiomba serikali kuingilia kati suala hilo.

Bernard Mwapinga alisema hawapingi mradi huo wa ujenzi wa barabara, lakini wanachotaka ni kuona wanatendewa haki kwa kulipwa fidia ya nyumba zao zinazotakiwa kubomolewa.

Akizungumzia malalamiko ya wananchi hao, Mratibu wa Tarura Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Gerard Matindi, alisema kabla ya kuanza mradi huo waliwashirikisha wananchi wa vijiji vyote vya mradi na wote wakakubali wenyewe kubomoa nyumba zao zilizo ndani ya hifadhi ya barabara hiyo bila fidia ili kupisha mradi huo.

Alisema wananchi wote wa kuanzia Inyala hadi Simambwe walikubali kupisha mradi huo bila kulipwa fidia na Tarura ilifanya vikao mbalimbali kujadili suala hilo.





## Hifadhi Msitu Jozani yatambuliwa rasmi kimataifa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kwamba tayari Hifadhi ya Msitu wa Jozani imetambuliwa rasmi kimataifa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni (Unesco) na kujumuishwa miongoni mwa hifadhi bora 100 zilizopo duniani.

Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema hayo ni mafanikio makubwa tangu kuanzishwa kwa hifadhi hiyo mwaka 1990 na kusajiliwa mwaka 1992.

Mjawiri aliwataka wananchi wanaoishi na kuzungukwa na hifadhi ya msitu wa Jozani vijiji saba kutambua sifa ya msitu huo kimataifa pamoja na kuchukua jukumu la kuulinda kutokana na vitendo vya uharibifu wa kimazingira.

Alisema vitendo vya uharibifu wa mazingira ikiwamo ukataji wa miti na uwindaji wanyama kinyume na sheria unaweza kuiondolea sifa msitu huo ambao kwa sasa umekuwa ukitembelewa na watalii wengi.

Alisema katika mwaka 2016 jumla ya watalii 50,000 walitembelea msitu huo huku idadi ikiongezeka katika mwaka 2019 na kufikia watalii 69,000.

Alisema msitu wa hifadhi ya taifa wa Jozani umetambuliwa rasmi kama hifadhi yenye kulinda viumbe mbalimbali adimu duniani.

Alieleza kuwa baadhi ya viumbe wanaopatikana katika hifadhi ya msitu wa Jozani ambao hawapatikani sehemu yoyote duniani ni Kima Punju.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba msitu wa hifadhi wa Jozani hivi sasa unatambuliwa rasmi na kuingizwa katika orodha ya hifadhi 100 bora duniani kutokana na kuhifadhi biaonuwai nyingi kwa wakati mmoja," alisema.

Mjawiri aliwataka wananchi wanaoishi na kuzungukwa na msitu wa hifadhi ya Jozani kulinda hifadhi hiyo na kujiepusha na vitendo vinavyohatarisha hifadhi hiyo ambayo inaweza kuwakosesha mapato wananchi.

Alisema katika kipindi cha miaka 10, wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo walipata mgawo wa zaidi ya Sh. bilioni 1.2 ikiwa ni mapato yanayoingia katika sekta ya utalii, huku sehemu wakipewa wananchi kutokana na athari wanazozipata.

Alizitaja athari wanazozipata wananchi wanaozungukwa na msitu wa hifadhi ni pamoja na mashamba yao kuvamiwa na kuharibiwa na Kima Punju na wanyama wengine waliomo katika hifadhi ambao hawatakiwi kuwadhuru.

Msitu wa Hifadhi ya Jozani uliopo Wilaya ya Kati Unguja, umezungukwa na wananchi wa vijiji vya Ukongoroni, Pete, Charawe, Unguja Ukuu pamoja na Muungoni na Binguni.

# ZSTC kununua mwani kwa wakulima

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amesema serikali imejipanga kuimarisha zao la mwani na sasa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC), litafanya ununuzi moja kwa moja kwa wakulima kama inavyofanya kwa upande wa karafuu.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza ari kwa wakulima wa mwani ambao asilimia 90 ni wanawake wa vijijini maeneo ya mwambao wa pwani ambayo ni maarufu kwa kilimo hicho.

Balozi Amina alisema hayo wakati akifanya majumuisho na kujibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia bajeti ya wizara hiyo na suala la maendeleo ya kilimo cha mwani vijijini lilichukuwa nafasi kubwa.

Alisema uamuzi huo lengo lake ni kuona kilimo cha mwani kinapata mafanikio makubwa na kinakuwa mkombozi kwa kinamama kujiajiri sekta binafsi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefikia maamuzi na kulitaka Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) kununua mwani wote kutoka kwa wakulima baada ya kutegemea ununuzi kwa watu binafsi," alisema.

Akifafanua alisema, serikali imechukua uamuzi huo, huku yakiwapo maandalizi ya ujenzi ya kiwanda cha kusarifu bidhaa zinazotokana na mwani kwa ajili ya kuongeza thamani na ubora wa zao hilo.

Alisema kiwanda cha kusarifu mwani na kuongeza thamani, kinatarajiwa kujengwa huko Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba.

"Maandalizi ya ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani yanakwenda vizuri ambacho ni mkombozi katika kukuza na kuimarisha kilimo cha mwani Zanzibar," alisema.

Alisema bei ya zao la mwani imeanza kuimarika na hivyo kuleta faraja kubwa kwa wakulima waliopo katika mwambao wa pwani na sasa kilo moja ni Sh. 14,000.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Biashara Viwanda kwa mwaka wa fedha 2020-2021, jumla ya Sh. 23,569,700,000 zitatumika kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka 2020-2021.



Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Mselem (kushoto), akizungumza na Mwakilishi wa Viti Maalum, Viwe Khamis, nje ya ukumbi wa baraza hilo, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yajipanga kuimarisha utalii majengo kale

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imejipanga kuimarisha na kutangaza utalii wa majengo ya kale kwa lengo la kuwawezesha watalii wanaokuja kujuwa historia ya makumbusho na watawala waliotawala Zanzibar.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akielezea juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Oman, kuimarisha mambo ya kale ikiwamo majengo ya historia na nyaraka.

Alisema Serikali ya Oman ndiyo iliyochukua jukumu la kuimarisha majengo ya historia pamoja na nyaraka za makumbusho ambayo ndiyo zinazoweza kubeba utalii wa Zanzibar na kuwawezesha wasomi na mabingwa wa fani mbalimbali kuja nchini na kusoma historia hiyo.

"Tunaipongeza kwa dhati Serikali ya Oman ambayo imechukua jukumu la kufanya ukarabati mkubwa wa jengo la historia kielelezo cha Zanzibar Beit-Al-Jaib liliopo Mji Mkongwe wa Zanzibar pamoja na nyumba ya nyaraka ya mambo ya kale iliyopo Kilimani," alisema.

Alisema nyumba ya nyaraka iliyopo Kilimani imepatiwa mitambo ya kuhifadhi nyaraka pamoja na kuwekwa vifaa ambavyo vitasaidia kuimarisha uhai wa nyaraka hizo na kuwa bora.

Pia, alisema ujenzi wa jengo la Beit-al-Jaib unaendelea vizuri chini ya ufadhili wa Serikali ya Oman ambayo imetoa jumla ya Sh. bilioni 13.

Kazi ya ukarabati wa jengo hilo imepewa kampuni moja kutoka Italia ya CGG ambayo imetakiwa kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia masharti ya miji iliopo katika urithi wa kimataifa.

Alisema ujenzi huo unafanywa chini ya uangalizi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Utamaduni na Sayansi (Unesco), kufuatia jengo hilo kuingizwa katika hifadhi ya urithi wa mambo ya kale.

Alisema jumla ya Sh. 2,400,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuyafanyia ukarabati mkubwa makumbusho ya mtawala wa kienyeji Mwinyimkuu yaliyopo Dunga, Wilaya ya Kati pamoja na Bi Hole, Bungi.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


### KUPOTEA KWA CHETI



**Meshack Sylvester Mbwaga** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato sita chenye index namba **S0142-0747** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shule ya Sekondari Galanos. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DSM/PHQ/RB/409948/2020.**

215760002

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT MOSHI**

**LAND CASE NO. 7 OF 2019**

**JACKLINE CHARLES NDEKILO............APPLICANT**

**VERSUS**

**BARCLAYS BANK &3 OTHERS.........RESPONDENT**

**TO: GILBERT GERVAS MASSAWE,**
**C/O WARD EXECUTIVE OFFICER,**
**NSARANGA-MOSHI.**

**NOTICE OF DATE MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on 14th day of Julay 2020 at 9:00am Before Honorable T. MWENEMPAZI JUDGE

AS WHERE: S ervice on you has been ordered to be published in the NIPASHE newspaper.

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the document upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER MY HAND THE SEAL OF THE COURT, this 21th day of MAY ,2020**

**O.H.KINGWELE**
**DEPUTY REGISTRAR**

115760302

---

### TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA

**SAMBO MASHALA JITOBA** MKAZI WA MAGANZO WILAYANI KISHAPU MKOANI SHINYANGA.
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YAKE YA **KIWANJA NAMBA 1010 KITALU "GG-HD"** KITANGILI KATIKA MANISPAA YA **SHINYANGA,** AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2020 MAENEO YA MAGANZO.
KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA SAMBO MASHALA JITOBA **KWA SIMU NAMBA 0766754409**
RB NAMBA **SHY/RB/2020,**
CONTROL NAMBA **9910812843204**

115760102

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ngunda Mchunga Mabula** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Landcruiser **VX** yenye namba za usajili **T 262 BBG.** Chassis No. **Zhj800017578.** Hivyo yeyote atakayeiona kadi hiyo apeleke taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo Mjini Bariadi. Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo, imetolewa katika kituo cha polisi cha Bariadi kwa namba **SIM/BAR/RB/420373/2020.**

115760802

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI.

**FRANK THOMAS MANYANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T789AXN,** NISSAN SAFARI.
ENGINE NO **ZD30(DDTi)2953**
CHASSIS NO **WTY61-000103**
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI - **ARU/ARU/RB/415542/2020** AU **PIGA SIMU 0757 590 283.**

115760701

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ATHANAS RAPHAEL MUSSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina Toyota Passo yenye namba za usajili **T976 CYM.** Chassis no. **QNC100038248,** Engine no. **K31382837.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/418063/2020**

115760602

---


**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO**

**KWA BEI**

**NAFUU SANA**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Sido kuendeleza majengo wajasiriamali kuchakata mazao

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

KAIMU Mkurugenzi wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), Shoma Kibende, amesema wameanza mpango wa kuendeleza ujenzi wa majengo ya viwanda katika maeneo yao kwenye mikoa 25 wanayotoa huduma ili kuwezesha wajasiriamali kupata sehemu za kuchakatia mazao ghafi.

Akizungumza jana wakati wa kukagua ujenzi wa moja ya jengo la kiwanda mkoani Kigoma, Kibende alisema kufikia mwezi Juni wameshatenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa majengo manne katika mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Kigoma.

Alisema wanatarajia majengo hayo kukamilika Juni 30 na kuwataka wananchi walio tayari kuanza kutuma maombi ili yatakapo kamilika uzalishaji uanze mara moja.

"Mkakati wetu ni kuhakikisha viwanda vinaanzishwa na kukuza vilivyopo ili mazao tunayozalisha nchini yaweze kuchakatwa na kuuzwa kama bidhaa badala ya malighafi," alisema.

Naye Meneja wa Sido, Mkoa wa Kigoma, Gervas Tahamba, alisema ujenzi wa jengo la kiwanda katika Mkoa wa Kigoma, unagharimu Sh. milioni 200 na wanatarajia mwishoni mwa mwezi huu utakamilika.

Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Samson Anga, aliushauri uongozi wa Sido kuandika maandiko yatakayo wawezesha kujenga majengo mengi yatakayotumika kwenye uzalishaji wa bidhaa.

"Veta wanafundisha Sido, mnakuja kutoa maeneo ya kazi hiyo ndiyo kazi yenu tekelezeni," alisema.

Ujenzi wa majengo hayo unatekelezwa kupitia fedha za serikali za maendeleo lengo likiwa ni kuwezesha uchakataji wa mazao makubwa kama korosho na michikichi yaweze kutoa tija.

# Wawekezaji wahakikishiwa umeme uhakika Kisarawe

**Na Romana Mallya**

WILAYA ya Kisarawe imewakaribisha wawekezaji kwenda kuwekeza baada ya kutekeleza agizo la Rais John Magufuli kwa kuhakikisha huduma muhimu ikiwamo umeme inapatikana kwa uhakika.

Mkuu wa wilaya hiyo, Jokate Mwegelo, aliwakaribisha wawekezaji kwenda wilayani humo juzi baada ya kutembelea kiwanda cha Mkongoma General Suppy, kinachojihusisha na uzalishaji wa chaki zinazosambazwa maeneo mbalimbali nchini.

Kiwanda hicho kipo Kata ya Msimbu, Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani, ambacho awali kilikuwa kinakabiliwa na changamoto ya umeme ambayo imetatuliwa na kukiwezesha kupunguza gharama za uzalishaji.

"Mwaka jana, Rais Magufuli alifanya kikao na wafanyabiashara na alielekeza viongozi wa mikoa, wilaya husika kusaidia wawekezaji kwenye maeneo yao kupata unafuu na changamoto za uendeshaji.

"Katika kipindi hicho imekuwa ni faraja kubwa kwetu tulipata meneja wa Tanesco ambaye siyo goigoi, changamoto kubwa wilaya ya Kisarawe ilikuwa ni upatikanaji wa umeme kwenye viwanda.

"Changamoto nyingine ilikuwa ni maji na barabara ingawa hii ya barabara kidogo inavumilika ikilinganishwa na umeme na maji."

Mwegelo alisema Mkongoma ni kijana mzawa ambaye ameamua kuunga mkono azma ya Rais Magufuli ya kuhakikisha nchi inakwenda kwenye uchumi wa kati wa viwanda, kwa kuamua kuzalisha chaki ambazo zinasambazwa nchi nzima.

"Mkomboma ametuambia hapa amekuwa akihangaika ndani ya miaka sita, Mkuu wa mkoa aliwahi kufika na kutoa ahadi umeme, Naibu Waziri wa Nishati naye alifika na kumuahidi, na wewe umekuwa ukizungumzia adha ya nishati namna ilivyokuwa ikiongeza gharama za uzalishaji," alisema.

Alisema mwekezaji huyo alikuwa akitumia siyo chini ya Sh. milioni sita kununua mafuta ya dizeli ili kuendesha kiwanda hicho, lakini tangu umeme umefika anatumia Sh. 400,000 pekee kwa mwezi.

"Tanzania ya umeme inawezekana, ndiyo maana Rais Magufuli amejikita kwenye uboreshaji wa nishati ya umeme, ikipatikana gharama za uzalishaji zinashuka ndiyo maana kuna bwawa la Nyerere, Rufiji litakalozalisha Megawati 2, 115," alisema.

Alimpongeza mwekezaji huyo kuongeza uzalishaji kwa sababu shule zitakapofunguliwa uhitaji utaongezeka.

Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Geoffrey Mkomboma, aliahidi shule za wilaya hiyo zitakapofunguliwa kiwanda chake kitaunga mkono sekta ya elimu kwa kugawa chaki shuleni.

"Uwezo wa kiwanda chetu tunazalisha katoni 200 au 300 inategemea na msimu, shule zitakazonufaika ni zile zote zinazopewa fungu na serikali ndiyo tutakazozipa chaki ni shule 200 zitakazopewa zawadi ya katoni moja moja," alisema.

Meneja wa Tanesco Wilaya ya Kisarawe, Nyanda Mlagwa, alisema wanaendelea kupelekea huduma maeneo mbalimbali Kisarawe na kuwataka wawekezaji waende wilayani humo kuwekeza.

Alisema hadi mwezi Oktoba, mwaka huu usambazaji wa umeme utabaki kwa vijiji 13 kati ya 84 wilayani humo na ifikapo mwezi Juni mwakani, vyote vitakuwa vimefikiwa.




Katibu Tawala Msaidizi wa Kilimo na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, akikabidhi kifaa saidizi kwa mmoja wa mawakala wa kampuni ya YARA Tanzania, Abiudi Mwatebela, kutoka Rungwe ikiwa ni sehemu ya msaada kutoka kampuni hiyo ili mawakala hao na wakulima waendelee kujikinga na maambukizo ya Covid-19. Kushoto ni Benson Sanga wa ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na mwakilishi wa YARA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, John Rotich. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aelekeza wawekezaji upatikanaji cheti mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mussa Sima, amewataka wawekezaji kuwasiliana na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) au kutumia wataalamu elekezi wenye weledi kurahisisha upatikanaji wa cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA).

Sima ameyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipotembelea kiwanda cha Tropical Int. Group Inc kinachozalisha nyaya za umeme pamoja na transfoma na kusema Bunge na Kamati ya Kudumu ya Nishati vimeelezwa kwamba kiwanda hicho hakina cheti cha EIA.

"Nimefika kutembelea kiwanda hiki na timu ya wataalamu kutoka NEMC kuona kama kilichosemwa Bungeni ni cha kweli. Tumebaini changamoto kadhaa na kushauri namna nzuri ya kufanyakazi ili lengo letu la kuwafanya wawekezaji waendelee na shughuli zao bila kukata tamaa lifanikiwe. Hata hivyo, tunategemea wawekezaji wafanye shughuli zao bila kuathiri mazingira," alisema.

Waziri Sima aliwataka wawekezaji kuwasiliana na NEMC moja kwa moja kwa kuwa Baraza hilo limerahisisha sana upatikanaji wa huduma zake ikiwamo utoaji wa cheti cha EIA badala ya kutumia wataalam elekezi wasio waaminifu ambao wamekuwa wakichelewesha mambo muhimu kwa wawekezaji.

"Aidha Waziri Sima amewakumbusha wenye viwanda kuwa ni makosa kuendelea kufanya uzalishaji kabla ya kufanya EIA kwani kufanya hivyo kunaleta athari nyingi katika mazingira

"Naendelea kutoa wito kwa wenye viwanda kufanya kazi kwa karibu na NEMC kwa kuwa kila kitu kimerahisishwa na kama watatumika wataalamu elekezi basi watumike wale wenye weledi unaoendana na mradi husika," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema licha ya kufanyia kazi maelezo ya waziri, baraza litakuwa karibu na wawekezaji kwa kuwashauri na kuwarudisha katika mstari wale wote ambao watakuwa wanakiuka sheria na kanuni za mazingira.

" Tutafanyia kazi maelezo yote ambayo Waziri ameelekeza kwa Baraza na hatutakuwa kikwazo katika kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini," alisema.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Charles Mlawa, alisema ujio wa waziri kiwandani hapo umewapa fursa kubwa ya kufahamu namna nzuri ya kuendesha kiwanda chao na kwa kufuata kanuni na sheria za mazingira.



# SANE ANAKUBALIKA POPOTE - RAIS BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

RAIS wa Bayern Munich, Herbert Hainer, amebainisha mpango wa klabu yake kumwania Leroy Sane, huku akisema hakuna timu ambayo isingependa kuwa na winga huyo wa Manchester City.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Sane kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na Bayern, na Agosti mwaka jana alikaribia kusajiliwa, kabla ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kuumia mguu wakati wa mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool.

Sane hajacheza mechi yoyote ya kiushindani tangu hapo, lakini Bayern wanampango wa kumsajili mchezaji huyo wa zamani wa Schalke ili arudi kule Bundesliga.

"Leroy Sane ni mchezaji mzuri, kila timu ingependa kuwa naye," alisema Hainer akiiambia BR.

"Inajulikana kwa mwaka sasa kwamba tunamtaka. Bado ana mkataba na Man City. Tumeonyesha vitu vinaendelea."

# Moratti: Inter haiwezi kumshikilia Martinez

**MILAN,** Italia

RAIS wa zamani wa Inter Milan, Massimo Moratti, amesema "huwezi kumshikilia mtu ambaye ana mawazo ya kuwa sehemu nyingine," wakati Lautaro Martinez akiendelea kuhusishwa na Barcelona.

Martinez amekuwa akitajwa kwamba anaondoka kwa miamba hao wa Serie A, Inter kwenda kwa mabingwa wa LaLiga, Barca, ambao wanataka kumsajili mchezaji huyo kama mrithi wa muda mrefu wa mshambuliaji wao, Luis Suarez.

Licha ya Barca kuripotiwa kwamba wamekuwa wakimwania tangu kabla ya mlipuko wa virusi vya corona, Mkurugenzi wa Michezo wa Inter, Piero Ausilio amesisitiza Martinez hatauzwa chini ya euro milioni 111 ambazo zipo kwenye mkataba wake.

Alipoulizwa kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, Moratti aliliambia gazeti la Sportmediaset: "Huwezi kumshikilia mtu ambaye ana mawazo ya kuwa sehemu nyingine.

"Ni ngumu kuendelea kuwa na mtu ambaye anataka kuondoka, ni kazi kubwa sana."

Huku majaliwa na Martinez yakiwa shakani, nyota wa Brescia, Sandro Tonali amekuwa chaguo la kwanza kwa kikosi hicho cha kocha, Antonio Conte.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye anafananishwa na gwiji wa Italia, Andrea Pirlo, pia amekuwa akihusishwa kutakiwa na Juventus na Manchester United.





# *Coutinho anataka kurudi zake EPL*

**MUNICH,** Ujerumani

PHILIPPE Coutinho anapanga kurudi kwenye Ligi Kuu ya England, kwa mujibu wa wakala wake, Kia Joorabchian.

Coutinho alikuwa nyota pale Liverpool, lakini akashindwa kujiimarisha yeye mwenyewe kule Barcelona baada ya uhamisho wa euro milioni 145 Januari 2018.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alijiunga na Bayern Munich kwa mkopo Agosti mwaka 2019 na amefunga mabao nane katika mechi 22 za Bundesliga msimu huu.

Huku Coutinho akiwa nje kuguza majeraha, inaonyesha wazi kwamba Bayern hawana mpango wa kumnunua moja kwa moja kwa euro milioni 120 zilizopo kwenye mkataba wake, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zikiwamo Tottenham, Arsenal na timu yake ya zamani ya Liverpool, zikiripotiwa kumuwania.

Joorabchian, ambaye ni wakala wa wachezaji wengine wa Brazil, David Luiz na Willian, sasa amethibitisha kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anapanga kurudi England.

"Anampango wa kurudi Ligi Kuu ya England," alisema Joorabchian akiiambia Sky Sports.

"Inaweza isitokee mwaka huu, lakini inaweza kutokea, hatuwezi kujua. Hatujajadiliana kitu chochote kwa sasa."

Hata hivyo, Joorabchian amesisitiza mazungumzo ya Barca ya kuweka pauni milioni 70 kama thamani ya Coutinho, au kumtoa kwa mkopo kwa pauni milioni 9 yanaendelea.

# KANE ATAKA KUIONA SPURS IKIFUZU UEFA



**LONDON,** England

HARRY Kane amesema timu yake ya Tottenham Hotspur inahitaji kushinda mechi nane kati ya tisa walizobakiza kwenye Ligi Kuu England ili kupata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Spurs wapo kwenye nafasi ya nane katika msimamo, pointi saba nyuma ya timu inayoshika nafasi ya nne, Chelsea, lakini baada ya janga la corona kupita na ligi kutarajia kurudi upya, wanaamini watapambana kufanikisha hilo.

Straika Kane, Son Heung-min na Steven Bergwijn, wote walipata majeraha ambayo yalitishia uwezekano wao wa kucheza tena msimu huu, sambamba na Moussa Sissoko, lakini baada ya ligi kusimama kutokana na janga la corona kwa zaidi ya miezi miwili, wakali hao sasa wapo fiti kwa ajili ya kuipambania timu yao.

Kane alisema: "Tunapaswa kumalizia kwenye nne bora, hakuna ubishi wa hilo. Tuna mechi ngumu dhidi ya Manchester United, lakini ukweli ni kwamba tunahitaji kushinda mechi saba au nane ili kupata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Ufiti wa Kane utakuwa muhimu zaidi kwa Spurs, baada ya kupata majeraha ya misuli yaliyomfanya awe nje ya uwanja tangu siku ya mwaka mpya. Lakini, kwa sasa yupo vizuri na alisema: "Ilikuwa jambo zuri kupata yale mapumziko.

"Sijacheza mechi kwa miezi sita sasa, ni muda mrefu sana. Kuhusu kuwa majeruhi, sasa hivi nipo fiti."

## Kompany akataa kumrithi Arteta City

**MANCHESTER,** England

VINCENT Kompany amekataa nafasi ya kurudi Manchester City kwenda kujiunga na benchi la ufundi na badala yake ameamua kubaki Anderlecht.

Nahodha huyo wa zamani wa Man City, alipata ofa ya kurejea kwenye klabu hiyo kujumuika katika benchi la ufundi ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kuondoka.

Kocha Pep Guardiola amekuwa akitafuta msaidizi wa kuziba pengo la Mikel Arteta, aliyetimka kwenda kuchukua mikoba ya kuwa kocha mkuu kwenye kikosi cha Arsenal, Desemba mwaka jana.

Kwenye kikosi hicho, Kompany amekuwa na kazi kubwa baada ya kushinda mataji 10 katika miaka 11 aliyodumu na timu hiyo, huku sehemu kubwa akiwa nahodha.

Hata hivyo, mapema wiki hii, Kompany aliithibitishia Anderlecht kwamba amejitolea kwa nguvu zote kubaki kwenye timu hiyo hadi mkataba wake utakapofika tamati 2022 na kuendelea.

Ripoti zinadai kwamba moja ya sababu zinazomfanya Kompany agome kurudi Etihad kwa sasa ni kuhusu mpango wake wa kutaka kuendelea kucheza baada ya kuona majeraha yamemharibia sana, kitu ambacho anaamini akirudi Man City hatapata nafasi ya kufanya hivyo.



## *Inter Milan kumbakiza Sanchez*

**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter Milan imethibitisha kwamba, Alexis Sanchez ataendelea kubaki kwenye kikosi hicho hadi mwisho wa msimu huu wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Mshambuliaji huyo wa Manchester United, Sanchez yupo kwa mkopo kwenye kikosi cha miamba hiyo ya Serie A tangu wakati wa majira ya joto mwaka jana na alipaswa kurejea Old Trafford mwezi ujao.

Serie A, ilisimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, hivyo jambo hilo lingemfanya Sanchez kuachana na timu hiyo ya San Siro kabla ya msimu kumalizika kwa sababu mkataba wa mkopo utakuwa umefika mwisho.

Mkurugenzi wa Michezo wa Inter Milan, Piero Ausillo, alisema nyota huyo wa zamani wa Arsenal atapewa nafasi ya kuthibitisha uwezo wake kwamba anastahili kuongezewa muda zaidi.


Majeraha yamekuwa yakimwandama Sanchez huko Italia, ambapo amefunga bao moja tu katika mechi 15 alizochezea kikosi hicho kinachonolewa na kocha Antonio Conte.

Lakini Ausillo alisema kuhusu Sanchez: "Ataendeelea kubaki hapa hadi mwisho mwa msimu na baada ya hapo tujadili hatima yake na Manchester United. Hii ni nafasi kwake ya kutuonyesha uwezo wake."



## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# IGHALO ABAKIZWA UNITED HADI 2021

**Imekuwa ni ndoto kwa upande wake na ninamatumaini atamaliza kile...**

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imefanikiwa kuongeza muda wa kucheza kwa mkopo wa Mnigeria Odion Ighalo kutoka Shanghai Shenhua ya nchini China hadi Januari 2021.

**Ighalo alijiunga na United Januari, huku akifunga mabao manne kwenye mechi nane alizocheza katika mashindano yote kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria muda wake wa kukaa hapo ulikuwa unamalizika Mei 31, mwaka huu na sasa United wamekubaliwa kumbakisha hapo kwenye dimba la Old Trafford hadi Januari 31, mwakani.

Straika huyo wa zamani wa Watford, Ighalo - ambaye ni shabiki wa United tangu utotoni - hajaanza katika mchezo wowote kwenye Ligi Kuu ya England, lakini alifunga katika kila mechi aliyoanza kwenye Ligi ya Europa na Kombe la FA.

Akizungumza na MUTV wiki iliyopita, Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer alisema ana matumaini ya kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

"Usajili wake wa mkopo unakamilika Mei, lakini nina matumaini tutambakisha," alisema Solskjaer.

"Tupo katika majadiliano. Wamekuwa waungwana kwetu, na wamemruhusu kuichezea klabu ya ndoto zake.

"Imekuwa ni ndoto kwa upande wake na ninamatumaini atamaliza kile alichokianza, kwa matumaini na taji kwa upande wetu."

Msimu wa Ligi Kuu ya England unatarajiwa kuendelea Juni 17, mwaka huu, huku timu zikiwa zimerudi kwenye mazoezi wiki iliyopita.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA KWA WERNER

CHELSEA inafikiria kuanza mpango wa kumsajili straika wa RB Leipzig, Timo Werner mwenye umri wa miaka 24, kama raia huyo wa Ujerumani akionyesha nia ya kutaka kuhama. ***(ESPN)***

### MESSI, BARCA HADI 2021

MSHINDI mara sita wa Ballon d'Or, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 32, atabaki Barcelona msimu ujao, huku mkataba wake ukionyesha kwamba mchezaji huyo wa Argentina anaweza kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto akiwa huru. ***(Standard)***

### WILLIAN AKATALIWA REAL

REAL Madrid imekataa nafasi ya kumsajili winga wa Chelsea, Willian mwenye umri wa miaka 31, akiwa mchezaji huru. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mkataba wake pale Stamford Bridge unamalizika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### YAFUNGA NYOTA WAKE

LIVERPOOL ipo kwenye majadiliano ya kuongeza mkataba wa mkopo kwa kiungo wa kimataifa wa Wales, Harry Wilson mwenye umri wa miaka 23, pale Bournemouth na straika wa Uingereza, Rhian Brewster mwenye umri wa miaka 20, kule Swansea hadi mwisho wa msimu. ***(Telegraph)***

### LUIZ KUFUNGWA ARSENAL

ARSENAL ipo tayari kumpa ofa mlinzi wa kimataifa wa Brazil, David Luiz mwenye umri wa miaka 33, mkataba wa mwaka mmoja, lakini itampunguzia mshahara wake wa pauni 130,000 kwa wiki. ***(Mirror)***

### GARETH KUISUSIA EPL

KOCHA wa timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate hatahudhuria mechi za Ligi Kuu ya England wakati msimu huo utakaporejea tena, kwani anahisi uwapo wake si kitu muhimu. ***(Star)***

### MAKOCHA EPL KUHOJIWA

KLABU za Ligi Kuu ya England zitajadili uwezekano wa makocha wao kuhojiwa na televisheni wakati wa mapumziko katika mkutano wa kesho Alhamisi. ***(Express)***

### CHELSEA YATAKA 9 BENCHI

KLABU ya Chelsea imetuma maombi kwenye Ligi Kuu ya England kuongeza idadi ya wachezaji wa akiba kwenye benchi kutoka saba hadi tisa kwa kipindi cha msimu kilichobakia. ***(Mail)***

### EVERTON YAITA KIPA

KLABU ya Everton inatarajiwa kumuita tena mlinda mlango, Jonas Lossl mwenye umri wa miaka 31, baada ya mkataba wake wa kucheza kwa mkopo kumalizika katika klabu ya Huddersfield Town. ***(Yorkshire Evening Post)***

### CELTIC YAMGEUKIA BRAVO

CELTIC wanafikiria kumsajili mlinda mlango wa Manchester City raia wa Chile, Claudio Bravo mwenye umri wa miaka 37. ***(Times)***

HABARI MICHEZO

## Malale alia nyota kuongezeka uzito

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Polisi Tanzania, Malale Hamsini, ameeleza kusikitishwa kwake kutokana na baadhi ya wachezaji wake kufanya uzembe wa kutokufanya mazoezi pamoja na kufuata programu alizowaachia katika kipindi chote walichokuwa wamepumzika baada ya kuibuka kwa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Akizungumza na Nipashe jana asubuhi kutoka Moshi mkoani Kilimanjaro, Malale alisema wachezaji hao wamerudi wakiwa wameongezeka uzito pamoja na kuonekana wazi walikuwa wamejiachia, kitu ambacho kinaweza kuwakosesha kupata nafasi ya kupangwa mara kwa mara.

"Kuna wachezaji ambao wamefanya uzembe, hawajafuata maelekezo ambayo nilikuwa nawapa wakiwa majumbani hata ukiwaangalia wamepoteza mwonekano wa mazoezi jambo hilo limenikwaza," alisema Malale.

Hata hivyo, licha ya Nipashe kumtaka Malale kuwaanika wachezaji hao, alisema hawezi kuwataja kwani itawapa wakati mgumu katika kipindi chote na kukosa ari uwanjani.

"Siwezi kukutaji ni siri ya klabu nina kazi kubwa ya kuwarudisha kama walivyokuwa mwanzo, nawapongeza wale waliofuata maelekezo yangu vizuri," alisisitiza.

Alizungumzia ratiba iliyotolewa juzi na Bodi ya Ligi (TPLB), kupitia kwa Mtendaji wake Mkuu, Almas Kasongo, Malale alisema anaipongeza bodi hiyo kwa kuzipa klabu muda mrefu wa kujiandaa kabla ya kuanza kwa Ligi Kuu Juni 20, mwaka huu kwa timu ambazo hazina viporo.

Ligi hiyo itarejea rasmi Juni 13 kwa timu zenye viporo na zitaendelea kuvimalizia hadi Juni 17 kabla ya Juni 20, mwaka huu timu zote kushuka dimbani zikiwa mechi sasa, ambapo Polisi Tanzania itaikaribisha Lipuli FC kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

## TPLB, marefa wamalizana

**Na Faustine Feliciane**

ZIKIWA zimebaki siku tisa kabla ya kuanza kwa ligi za soka, Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili, Bodi ya Ligi nchini (TPLB), kupitia kwa Ofisa Mtendaji wake Mkuu, Almas Kasongo amesema wamemalizana na waamuzi wa ligi hizo kwa kulipa madeni yao.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kasongo alisema pamoja na kuwapo kwa changamoto ya rasilimali fedha, Shirikisho la Soka nchini (TFF), na TPLB kwa kutambua umuhimu wa waamuzi katika soka, wameamua kuwapa kipaumbele kwa kulipa madeni yao ya msimu wa 2019/2020.

"Tumetumia zaidi ya shilingi milioni 500 kulipa madeni kwa waamuzi wote wakiwamo wale ambao wanatumikia adhabu, tunataka kuona ligi inaanza, huku tukiwa hatuna madeni kwa waamuzi," alisema Kasongo.

Aidha, alisema kuwa ni matarajio yao kuwa sasa waamuzi watafika kwenye vituo kwa wakati na kuchezesha mchezo pasipokuwa na wasiwasi wa posho zao.

# KOCHA AZAM FC AIWAHI SIMBA DAR

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Kocha Mkuu wa Klabu ya Azam FC, Mromania Aristica Cioaba, amerejea nchini kuendelea na kibarua chake cha kuifundisha timu hiyo kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, huku pia akiiwahi mechi ya robo fainali ya Kombe la FA, kati ya timu yake dhidi ya Simba, hapo Juni 27, mwaka huu.

**Kwa mujibu wa mtandao rasmi wa Klabu ya Azam FC, Cioaba aliwasili nchini Jumatatu jioni akitokea kwao Romania alikokwenda baada ya kuzuka kwa ugonjwa wa Covid-19 duniani, unaosababishwa na virusi vya corona.**

Kocha huyo aliwasili pamoja na kocha wa viungo, Costel Birsan, wakitokea Frankfurt, Ujerumani ambako ndiko walikopata usafiri wa ndege ya kurejea Tanzania.

Makocha hao walikwama kurejea ndani ya muda kutokana na nchini kwao kuwapo kwa karantini ya ugonjwa huo.

Taarifa ya Azam imeeleza kuwa wawili hao walitarajia kuanza kazi jana jioni, huku kikosi hicho kikiwa tayari kilishaanza mazoezi Jumatano iliyopita chini ya Kocha Msaidizi, Mrundi Bahati Vivier. Azam itakuwa na kibarua cha Ligi Kuu Juni 14, mwaka huu itakapocheza kwenye uwanja wao wa nyumbani, Azam Complex dhidi ya Mbao FC kutoka Mwanza.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, anatarajiwa kuwasili nchini wiki akitokea nchini kwao Ubelgiji.

Kocha huyo naye alikwama kutokana na karantini ya ugonjwa wa corona nchini kwao, na kwa sasa mazoezi yanasimamiwa na Boniface Mkwasa.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, amesema utaratibu wote umeshafanyika na huenda wakawa naye wiki hii, hata wakasafiri naye mjini Shinyanga ambako Yanga inakwenda kucheza dhidi ya Mwadui FC kwenye Uwanja wa Kambarage mjini huko.

"Unajua usafiri kwa sasa si rahisi hivyo, anatoka kwao, anapitia Ujerumani ambako ndiko kuna usafiri wa kwenda Ethiopia, ndiyo aje Dar, husafiri tu hivi hivi, lakini ndani ya wiki hii tunatarajia atakuwa nchini na hata safari ya kwenda Shinyanga huenda tukawa naye," alisema Bumbuli.

Yanga itacheza mechi hiyo dhidi ya Mwadui Juni 13, mwaka huu.

TUMEREJEA...



Kocha Mkuu wa Azam FC, Mromania Aristica Cioaba (kushoto) na Kocha wa viungo wa timu hiyo, Costel Birsan, walipowasili jijini Dar es Salaam juzi, tayari kujiandaa kwa mechi za Ligi na Kombe la FA. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Klabu Ligi Kuu Z'bar zamjadili Rais ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UMOJA wa Klabu za Ligi Kuu Zanzibar umekutana jana na Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), lengo likiwa ni kujadili kiini cha kutokuwapo maelewano na Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa kikao hicho, Haji Kidali, alisema kikao hicho maalum ambacho kiliandaliwa na viongozi wa Umoja wa Klabu Zanzibar, kilitarajiwa kufanyika jana katika Ukumbi wa Mafunzo Mjini hapa.

Alisema umoja huo wa klabu ulitaka kujua kiini cha baadhi ya wajumbe hao wa kamati ya utendaji kuandika barua ya kutokuwa na imani na Rais wa ZFF, Kombo wakati kama kuna tatizo wangeweza kutumia njia ya kukutana na umoja huo ambao waliuchagua.

"Umoja wa Klabu ndio waliowachagua wajumbe wa Kamati ya Utendaji, kwa hiyo kama kulikuwa na tatizo ni vema wangetumia busara ya kutaka kukutana na umoja huo kueleza tatizo hili na kuona namna gani tunatatua kwa pamoja na kuyaweka mambo sawa, lakini kitendo cha kuandika barua na kusambaza nakala kila sehemu ndio umoja wa klabu tunataka kujua walikuwa na lengo gani," alisema.

Hata hivyo, alisema kikao hicho anamatumaini makubwa kitakuwa na mafanikio pamoja na kufikia muafaka wa kumaliza sintofahamu iliyojitokeza kati yao hadi kufikia hatua ya baadhi ya wajumbe kuandika barua hiyo ambayo kwao wao wameoana haikuleta taswira nzuri katika safari ya mafanikio ya Soka la Zanzibar ambalo mara nyingi kumekuwapo na mivutano isiyokuwa na maana.

# Michezo

Jumatano Juni 3, 2020

Nipashe




Ighalo abakizwa United hadi 2021

UKURASA 22

LIGI NA IJE TU...



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (mbele), ambaye anaongoza kwa ufungaji Ligi Kuu hadi sasa, akiwa mazoezini na wenzake wakati huu wakiendelea kujiandaa na ligi hiyo kwenye uwanja wao wa Mo Simba Arena jijini Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# Mmachinga ashukia wazawa kasi Kagere

## ●●● Awashangaa kulala na kuachia wageni kuendelea kukimbiza Ligi Kuu huku...

**Na Saada Akida**

HUKU akiwataka wachezaji wazawa kujitambua, kujitunza na kuthamini kazi yao kwa kuwa soka kwa sasa ni ajira kubwa inayolipa vizuri tofauti na zamani, mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Mohammed Hussein 'Mmachinga' amemtaja straika wa Simba, Meddie Kagere kuwa anaweza kuvunja rekodi anayoishikilia ya mabao mengi kwa msimu mmoja Ligi Kuu Bara.

**Mmachinga ndiye anayeshikilia rekodi ya mfungaji wa mabao mengi kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu Bara ambayo aliiweka mwaka 1999 kwa kucheka na nyavu mara 26 wakati huo akiichezea Yanga.**

Hata hivyo, mwaka 2006 kwenye ligi hiyo ambayo pia ilishirikisha timu 16, mshambuliaji wa Mtibwa Sugar, Abdallah Juma alikaribia kuivunja baada ya kufunga mabao 25, ambayo nayo mpaka sasa hakuna mchezaji yeyote aliyewahi kuyafikia.

Na hadi Ligi Kuu inasimama Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID-19), Kagere ndiye anayeshikilia ukinara wa mabao baada ya kucheka na nyavu mara 19, akifuatiwa kwa mbali na Reliants Lusajo wa Namungo FC, Yusuf Mhilu (Kagera Sugar) na Paul Nonga wa Lipuli FC ambao kila mmoja ana mabao 11.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mmachinga alisema kitendo cha wazawa kuonyesha kuridhika haraka na kuona soka ni kazi ya kawaida ni moja ya sababu ya kushindwa kufikia malengo yao.

Mmachinga alisema inashangaza kuona mfano mshambuliaji msimu huu akiibuka mfungaji bora, lakini msimu unaofuata anapotea kabisa kwa kushindwa kuendeleza rekodi yake.

"Soka la sasa ni tofauti na zamani, muda huu mpira ni ajira inayoingiza fedha nyingi, hivyo wachezaji wanatakiwa kuachana na dhana mbovu za kuridhika na walipo na badala yake wanapaswa kuthamini kazi yao na kuzingatia zaidi mambo ambayo mchezaji anatakiwa kuyafanya ili kulinda kiwango chake.

"Wasipokuwa makini na kutothamini kazi hii, basi wenzetu watakuja kufanya vizuri kama sasa hivi katika ufungaji bora ambapo Meddie Kagere atachukuwa tuzo mara mbili mfululizo," alisema.

Mmachinga alisema washambuliaji wazawa wanatakiwa kuiga mfano wa Kagere ambaye amekuja kufanya kazi na huenda msimu huu akafikisha idadi ambayo ameishikilia yeye kwa muda mrefu.

Ligi Kuu ambayo imebakiza takriban raundi 10 kabla ya kufikia ukingoni, inatarajiwa kurejea Juni 13, mwaka huu na Kagere ambaye ni raia wa Rwanda, anahitaji mabao saba tu ili kuivunja rekodi hiyo ya Mmachinga iliyodumu kwa miaka 21 sasa.

Simba iliyopo kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 71, itarejea katika ligi hiyo kwa kuikaribisha Ruvu Shooting Juni 14, mwaka huu, katika Uwanja wa Taifa ikiwa ni siku moja baada ya watani zao, Yanga waliopo nafasi ya tatu na alama zao 51, kumenyana na Mwadui FC katika dimba la Kambarage mjini Shinyanga.

# Morrison, Tshishimbi waitia hofu Yanga

**Faustine Feliciane na Shufaa Lyimo**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, akitarajiwa kurejea nchini wakati wowote wiki hii, msaidizi wake, Boniface Mkwasa amesema wachezaji nyota wa timu hiyo winga mshambuliaji Bernard Morrison na kiungo mkabaji Papy Tshishimbi, wameitia hofu timu hiyo baada ya kupata maumivu.

Mkwasa, jana aliwaambia waandishi wetu kuwa nyota hao wameonekana kuwa na majeraha na wanaendelea kuwaangalia kwa karibu.

"Si majeraha makubwa, tunaamini mpaka kufika Juni 13, watakuwa fiti na kusafiri nao kwenda Shinyanga kwenye mchezo wetu wa kwanza," alisema Mkwasa.

Kuhusu mchezo wao huo ambao utakuwa dhidi ya Mwadui FC, Mkwasa alisema wamejipanga kikamilifu kuelekea katika mchezo huo, licha ya kwamba wanatambua kucheza ugenini kuna changamoto zake. Mkwasa alisema anashukuru wachezaji wote walioripoti kambini wanaendelea vizuri isipokuwa hao wawili ambao wamepata maumivu kidogo mazoezini.

"Tumejipanga vizuri kukutana na Mwadui hatuibezi ni timu nzuri lengo letu ni kurudi na pointi tatu nyumbani," alisema Mkwasa.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, aliliambia Nipashe kuwa Kocha Mkuu, Eymael anatarajia kurejea nchini wakati wowote wiki hii kuendelea na majukumu yake.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042